# LANSING SCHOOL DISTRICT
# WANAFUNZI NA FAMILIA
# MWONGOZO

Mwaka wa Masomo wa 2023-24

Lansing©
School District
Familia

KUJALI · USHIRIKIANO · UBORA

**2023-2024**
**Bodi ya Elimu**

Rachel Willis
*Rais*

Robin Moore
*Makamu wa Rais*

Dr. Saturnino Rodríguez
*Katibu*

Missy Lilje
*Mweka hazina*

Dr. Farhan Bhatti
Dr. Caitlin Cavanagh
Guillermo Z. López
Dr. Deyanira Nevárez Martínez
Rosalyn Williams
*Wadhamini*

519 W. Kalamazoo St.
Lansing, MI 48933

**www.lansingschools.net**

# Yaliyomo

**Utangulizi 01-06**
Ujumbe kutoka kwa Timu ya Maafisa Watendaji 01
Utangulizi 02
Mfumo wa Great Schools 03
Kalenda ya Wilaya 04
Title IX 05
Nambari Muhimu za Msaada 06

**Matarajio 07-21**
Uraia 07
Kanuni za Uraia wa Shule 07
Chanjo Zinazotakikana 07
Nafasi Sawa ya Elimu 08
Kushirikishwa kwa Wazazi 08
Haki na Majukumu ya Wazazi na Wanafunzi 08-11
Ustawi wa Wanafunzi 11
Ripoti ya Lazima ya Unyanyasaji na Utelekezaji 11
Magonjwa na Majeraha 12
Sera na Sheria za Mahudhurio 12-14
Huduma za Nyumbani 14
Vijana na Watoto Wasio na Makao 15
Haki za Wanafunzi za Kujieleza 16
Hoja, Mapendekezo na Malalamiko ya Wanafunzi 16
Kijitabu cha Mavazi cha Wilaya Nzima 17
Kijitabu cha Wanafunzi cha Shughuli za Baada ya Masomo 17
Usambazaji wa Nyenzo Zilizochapishwa 18
Kanuni za Matumizi ya Vifaa vya Mawasiliano vya Elektroniki 18
Matumizi ya Teknolojia na Kanuni za Usalama 19
Sheria na Masharti ya Tabia Salama ya Basi la Shule 20
Taratibu za Tabia Salama ya Basi la Shule 21

**Hatua ya Kinidhamu 22-36**
Matokeo kwa Wanafunzi na Hatua za Kurekebisha Tabia 22
Hatua ya Kurekebisha Tabia 22
Wazazi Kuarifiwa 22-23
Kanuni za Kurejesha Maadili 23-24
Ukaguzi na Upokonyaji 24-26
Ukaguzi wa Wanafunzi 24-25
Ukaguzi wa Makabati 25-26
Upokonyaji 26
Ukaguzi wa Magari 26
Kuingilia kati Kibinafsi au Kutengwa na Wafanyakazi 27
Tabia Ambazo Zinaweza Kusababisha Hatua za Kinidhamu 28-32
Kuondoshwa 32-33
Kuondoshwa na Mwalimu Darasani 33
Mwongozo wa Kuondoshwa Darasani 33
Kupelekwa kwenye Ofisi ya Utamaduni wa Shule 33
Kufukuzwa 34-35
Kufukuzwa Kulikoamrishwa na Jimbo 34
Mambo ya Lazima ya Kuzingatia 34-35
Kuondoshwa kwa Muda Kusiko kwa Lazima 35
Taratibu za Rufaa 36
Kiwango cha Shule cha Kuondoshwa kwa Muda 36
Maamuzi ya Ofisi ya Utamaduni wa Shule 36
Maamuzi ya Timu ya Ushauri 36
Kurejeshwa 36

**Mwongozo wa Nidhamu 37-38**
Hali ya Nidhamu 37
Kiwango cha 1: Hatua Zinazoelekezwa na Walimu/Wafanyakazi 37
Kiwango cha 2: Hatua Zinazoelekezwa na Wasimamizi 37-38
Kiwango cha 3: Shule Mbadala 38
Kiwango cha 4: Kuondoshwa kwa Muda Shuleni 38
Kiwango cha 5: Matokeo/Mipango Mbadala 38
Kiwango cha 6: Mkutano wa Kufukuzwa/Kufukuzwa 38
Maafisa wa Wilaya wa Utekelezaji 38

**Hatua za Kinidhamu 39-42**
Hatua za Kinidhamu za K-8 39
Hatua za Kinidhamu za 9-12 40
Nidhamu kwa Wanafunzi walio na Mipango ya IEP na 504 41-42

**Nyongeza 43-44**
Kanuni ya maadili Mema ya Masomo ya Mtandaoni 43
Matumizi Yanayofaa ya Teknolojia 43
Matarajio na Adabu za Wanafunzi 43-44
Hatua ya Kinidhamu 44
Majukumu ya Wazazi/Walezi 44

## Ifahamu Timu ya Wasimamizi Wakuu!



Ben Shuldiner
**Msimamizi**



Sergio Keck
**Naibu Msimamizi wa Wahusika Maalum na Mipango**



Jessica Benavides
**Naibu Msimamizi wa Shule**



Cordelia Black
**Mkurugenzi Mtendaji wa Utamaduni wa Shule na Hali ya Anga**



Kim Adams
**Msaidizi wa Msimamizi wa Fedha na Bajeti**



Kristina Tokar
**Afisa Mkuu Mtendaji**

# Ujumbe kutoka kwa Wasimamizi Wakuu

Wapendwa Wanafunzi na Familia,

Karibu kwenye Wilaya ya Shule za Lansing na pongezi kwa mwaka mzuri wa masomo wa 2023-2024! Kwa niaba ya usimamizi na wafanyakazi, tunajivunia na kufurahi kuwa na wewe kama mwanafunzi. Iwe we ni mwanafunzi mgeni au anayerejea, tunatazamia kuwa na mwaka wenye ufanisi pamoja.

Wilaya ya Shule ya Lansing imejitolea kuwahusisha wanafunzi katika matukio ya maana na yenye changamoto katika mazingira yanayokuza shauku ya kukua kibinafsi na ufanisi wa elimu. Tunajivunia kutoa nafasi mbalimbali za kielimu na shughuli za baada ya masomo zilizodhamiriwa kuboresha uzoefu wako wa shule na kupanua mipaka yako. Ufanisi shuleni na wa baadaye ni juhudi ya pamoja kati yako, wafanyakazi wa shule na familia yako. Tunakuhimiza ufaidike na nafasi nyingi na za kipekee ambazo tunazitoa ili ufikie malengo yako.

Lengo la kijitabu hiki ni kukupa rejeleo la mwongozo wa wilaya. Tunapendekeza kwamba familia zichukue muda kupitia kijitabu hiki kwa pamoja. Maelezo yaliyo katika mwongozo huu yanapatikana pia kwenye tovuti yetu katika www.lansingschools.net.

## Dhamira Yetu

Kudumisha elimu ya kiwango cha juu katika mazingira salama na ya kukuza yanayowasaidia wanafunzi wote kuishi maisha ya furaha na yenye maana.

## Maono Yetu

Mazingira bora zaidi, jumuishi na ya kielimu ambako watu wanafanya kazi pamoja katika jumuiya yetu yenye tamaduni nyingi na yanalenga kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya uraia muhimu wenye hima.



# Introduction

Bodi ya Elimu inachukulia kwa makini sana wajibu wake wa kuhakikisha mazingira mazuri na salama kwa wanafunzi na wafanyakazi wake. Mazingira yenye heshima ni muhimu kwa mchakato wa elimu. Bodi ya Elimu ilianza kutumia Kijitabu hiki cha Wanafunzi ili kutoa viwango na miundo inayofaa kukuza mazingira hayo salama ya elimu ambapo wanafunzi wanaweza kujifunza huku wakikomaa kiakili, kimwili, kihisia na kijamii. Kanuni zifuatazo zilitumika katika kutengeneza kijitabu hiki cha Wanafunzi:

1. Kijitabu hiki kinatoa mpangilio unaofaa kwa masomo. Ukosefu wa mpangilio huingiliana na lengo la elimu. Hata hivyo, Kijitabu hiki hakipaswi kuzuia ubunifu au furaha ya kusoma.
2. Kijitabu hiki kinalinda haki ya wanafunzi na wazazi huku pia kikikubali wajibu wao wa kuwa raia wazuri.
3. Kijitabu hiki kinajumuisha mwongozo wa kushughulikia tabia zinazotatiza (tazama ukurasa wa 19-22) kabla ziwe mbaya zaidi. Kanuni hizi hazilengi kutatua matatizo mabaya zaidi ya utovu wa nidhamu wa wanafunzi tu.
4. Mchakato huu umeundwa kwa msingi wa walimu, walimu wakuu, wanafunzi, wazazi kuheshimiana. Mchakato huu hauhatarishi hadhi ya mtu binafsi.
5. Wazazi wanawajibika kwa tabia za wanafunzi wao na lazima wahusike katika kutatua matatizo ya wanafunzi. Wanafunzi ambao wamefikisha umri wa miaka 18 wanaweza kuchagua kuwajibika kwa tabia zao wenyewe.
6. Wanajamii wote wa shule, pamoja na wanafunzi, walihusika katika kutengeneza Kijitabu hiki.
7. Kijitabu hiki kinazingatia umuhimu wa kanuni za haki za kurejesha maadili na Misaada Chanya ya Kuingilia Kati Tabia kama msingi wa kushughulikia tabia mbaya na kukuza utamaduni na mazingira mazuri ya shule.

Kijitabu hiki kinatimiza sera zote muhimu za Idara ya Elimu ya Michigan na hata pia sheria za jimbo na serikali kuhusu kuwatia nidhamu wanafunzi wa elimu ya kawaida/elimu maalum. Kijitabu hiki hakiondoi haki za mchakato wa kisheria chini ya sheria za serikali au jimbo za wanafunzi ambao wamebainika wanastahiki mipango na huduma ya elimu maalum au mabadiliko yanayofaa kwa ulemavu wao.

Msimamizi wa Shule atakuwa na wajibu mkuu wa kutumia Kijitabu hiki kwa njia thabiti, na ya haki na inayofaa katika wilaya nzima ya Shule ze Lansing.


## Katika Kijitabu hiki chote, Neno:

- **Mzazi** litamaanisha "mzazi au mlezi wa kisheria."
- **Mwalimu Mkuu** litamaanisha "mwalimu mkuu au mwakilishi wake."
- **Mwalimu** litamaanisha "mwalimu, mwakilishi wa mwalimu wa shule, au mwakilishi wa mwalimu wa muda mrefu."

## Wanafunzi wa K-12

Ndiposa kudumisha mazingira mema ya shule ya masomo, Kanuni Moja ya Nidhamu yenye Viwango vya Hatua za Utovu wa Nidhamu imetengenezwa. Mwalimu mkuu atawaarifu wazazi/walezi kuhusu kuondoshwa kokote muda kabla ya kufanyika. Mwanafunzi atapewa kazi za nyumbani wakati wa kipindi cha kuondoshwa kwa muda ili akamilishe na awasilishe kwa mwalimu wa darasa siku ya kurudi shule. Kumbuka: wilaya ina haki ya kupendekeza hatua zaidi kali za nidhamu kulingana na hali ya ukiukaji

Ni muhimu kwa wanafunzi na Wazazi/Walezi kuelewa kwamba kutofuatilia tabia inayotarajiwa kunaweza kusababisha hatua ya kinidhamu. Hatua ya kinidhamu katika Viwango vya I hadi V itachukuliwa katika kujibu utovu wa nidhamu wa mwanafunzi kulingana na mapendekezo ya msimamizi. Mwalimu mkuu (au mwakilishi wake) anawajibika kupendekeza hatua zote za nidhamu, ikiwemo mpango wa Kuondolewa kwa Muda Darasani/Shuleni. Katika kila hali, swali la kama kitendo cha utovu wa nidhamu kilifanya au la ambacho kinapaswa kuchukuliwa hatua ya nidhamu kitaamuliwa na utawala, na msimamizi wa shule au afisa wa usikilizaji.




# Mfumo wa Great Schools

## Imani

Kila mtu hujitahidi kutimiza lengo la pamoja la kuboresha matokeo ya wanafunzi, kuwaandaa wanafunzi kufanikiwa shuleni na baada ya shule. Kwenye jumuiya yote ya shule, kuna heshima. Wafanyakazi wa shule, wazazi, wanafunzi na wasimamizi wanaheshimiana.

## Usawa

Kila mtu hujitahidi kushughulikia usawa katika shule na matokeo yetu. Wanafunzi na familia kutoka kwenye jamii zilizotengwa wanahisi kujumuishwa, kuheshimiwa na wanaweza kutimiza malengo yetu ya pamoja kwa wanafunzi.

## Uongozi Thabiti wa Shule

Wasimamizi ni vielelezo vya uongozi na huendeleza ukuaji wa kitaalamu kwa walimu na wafanyakazi, hubuni na kutoa usaidizi wa maelekezo na wa hisia za kijamii unaosababisha mafanikio kwa wanafunzi.

## Miungano Thabiti ya Jumuiya na Familia

Uongozi wa shule hutoa raslimali kwenye jumuiya hadi kwenye majengo ya shule kwa kukaribisha, kuhimiza, na kubuni ushirikiano na familia, biashara na mashirika ya kijamii.

## Maagizo Thabiti

Maagizo hubinafsishwa, yanajumuisha kila mtu, yanatia motisha na yanaambatana na Lengo la Pamoja. Viwango vya juu huwekwa katika kila darasa. Wanafunzi huhusishwa zaidi katika shughuli za kiakili na kukuza ujuzi wa kuchanganua kwa kina.

## Mazingira Yanayosaidia

Shule ina utamaduni wa shule na madarasa ambako wanafunzi wanahisi salama, kusaidiwa na kupewa changamoto na walimu na wanafunzi wenzao.

## Walimu Wanaoshirikiana

Walimu wanajitahidi kufikia mafanikio na uboreshaji wa madarasa na shule zao. Wana fursa ya kushiriki katika kuendeleza taalama kwenye mazingira ya heshima na uboreshaji endelevu.

Imetolewa kwenye New York City Department of Education Framework for Great Schools, kutoka kwa utafiti wa University of Chicago Consortium on School Research.

## Mfumo wa Great Schools:

- Utaruhusu wilaya kubuni mbinu jumuishi, inayotokana na utafiti kwa usaidizi na uwajibikaji unaotambua na kuthamini mambo ambayo shule hufanya kila siku. Mbinu yetu itaheshimu dhana kwamba wanafunzi wanafanya mengi kuliko kando na mitihani.
- Utatoa usaidizi maalum kwa shule na kuzidisha jumuiya za mafunzo ya kitaalamu. Utahakikisha kuwajibika kwa shule na mfumo wa shule katika lengo la pamoja la kukuza walimu na wafanyakazi ili kuleta mafanikio kwa wanafunzi.
- Utabadilisha hamu ya mashindano na kuhimiza ushirikiano na lugha ya pamoja kwa ajili ya uboreshaji.
- Italeta pamoja uthabiti wa shule na jumuiya zao ili kuwasaidia wanafunzi katika siku za shule na baada ya siku za shule.
- Utaendeleza elimu kwa kuandaa kila mtu aliyehitimu katika shule ya umma ya Lansing ili kushindana katika nafasi za kazi za karne ya 21.

# Kalenda ya Wilaya

**AGOSTI**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | | |

**SEPTEMBA**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |

**OKTOBA**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | 31 | | | | |

**NOVEMBA**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | | |

**DESEMBA**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

**JANUARI**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | 31 | | | |

**FEBRUARI**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | | |

**MACHI**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

**APRILI**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | | | | |

**MEI**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | |

**JUNI**

| Jpl | Jtt | Jne | Jtn | Jne | Ijm | Jpl |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | | | | | | |

- ☆ Siku ya Kwanza ya Walimu
- ○ Siku ya Kwanza ya Shule (K-12, ECSE)
- Hakuna Shule (Zote)
- Siku Nusu (Shule ya Msingi)
- Siku Nusu (Zote)
- Siku Nusu ya Mtihani (Shule za Upili)
- Kuanza
- ○ Siku ya Mwisho ya Shule

Jisajili kwenye kalenda mahususi za wilaya na shule katika www.lansingschools.net

## Agosti
23 - Siku ya Kwanza ya Walimu
28 - Siku ya Kwanza ya Shule

## Septemba
01 - Si Siku ya Shule
04 - Leba Dei - Si Siku ya Shule
29 - Siku ya PD - Si Siku ya Shule

## Oktoba
20 - Siku ya PD - Si Siku ya Shule
31 - Siku Nusu (Shule ya Msingi)

## Novemba
07 - Siku ya Uchaguzi - Si Siku ya Shule
20 - Siku ya PD - Si Siku ya Shule
21-24 - Mapumziko ya Sikukuu ya Shukrani (Thanksgiving)
Si siku ya shule

## Desemba
25-29 - Likizo ya Majira ya Baridi
Si siku ya shule

## Januari
01-05 - Likizo ya Majira ya Baridi
Si siku ya shule
15 - Sikukuu ya Martin Luther King Jr
Si siku ya shule
17 & 18 - Mijarabu
Siku Nusu (Shule ya Upili)
19 - Maandalizi na Rekodi
Siku Nusu (Shule ya Zote)
26 - Siku ya PD - Si Siku ya Shule

## Februari
19 - Siku ya Marais
Si siku ya shule

## Machi
15 - Siku ya PD - Si Siku ya Shule
22 - Si Siku ya Shule
25-29 - Mapumziko ya Machipuko
Si Siku ya Shule

## Aprili
11 - Mijarabu ya SAT na ACT WorkKeys
Wachanga pekee A.M.
Wanafunzo Wote wa HS P.M.
Siku nzima kwa Shule ya Msingi

## Mei
10 - Siku ya PD - Si Siku ya Shule
24 - Maandalizi na Rekodi
Siku Nusu (Shule ya Msingi)
27 - Sikukuu ya Makumbusho (Mamorial)
Si siku ya shule

## Juni
05 & 06 - Mijarabu
Siku Nusu (Shule ya Upili)
07 - Siku ya Mwisho Shuleni
Siku Nusu
08 - Kuanza

**Darin Walter**
*Mratibu wa Title IX*
darin.walter@lansingschools.net
517-755-2037

**Erin Miracle**
*Afisa wa Kufuatilia Title IX*
erin.miracle@lansingschools.net
517-755-2010

**Masuala ya Title IX yanaweza pia kutumwa kama barua pepe kwa:**

Lansing School District
519 West Kalamazoo
Lansing, MI 48933

## Title IX ni nini?

Hamna mtu yeyote nchini Marekani, kwa misingi ya ngono, atatengwa asishiriki, au kunyimwa manufaa ya, au kubaguliwa katika mpango wowote wa elimu au shughuli ya kupokea usaidizi wa kifedha wa Serikali.
*20 U.S.C. § 1681, et seq.*

## Ufafanuzi wa Unyanyasaji wa Kingono

Shughuli isiyokubalika inayobainishwa na mtu mwadilifu kuwa hatari, mbovu, na inayokera kwa jumla, na inasababisha mtu akose uwezo sawa wa kufikia mpango au shughuli za elimu za shule.

# Title IX

## Mchakato wa Malalamiko ya Mada IX

**Madai ya Unyanyasaji wa Kingono (SH)**

**Tukio la Unyanyasaji wa Kingono Lilifanyika:**

- Shuleni?
- Kwenye basi au mbinu ya usafiri?
- Katika shughuli au tukio lililofadhiliwa na shule?

NDIYO

- Je, ni hatari, mbovu na inakera kwa jumla?

**na**

- inazuia mlalamishi uwezo wa kufikia shughuli au mpango wa wilaya au shule?

NDIYO

**Endelea chini ya Utaratibu wa Malalamiko ya Title IX**

**Rasmi/Si Rasmi**

HAPANA

**Hili Halikuwa Title IX SH**

- endelea chini ya Bodi ya Elimu au Maadili ya Matendo, ikiwezekana
- Kuondolewa kwa Lazima kwenye Title IX
- Sera au Mchunguzaji Tofauti

- sheria ya jimbo SH (ELCRA)
- uchokozi
- Unyanyasaji mwingine
- Maonyesho yasiyofaa ya mapenzi
- tabia mbaya ya kingono
- Kukosa ustaarabu

## DHULUMA NA MASHAMBULIZI

**Simu ya Moja kwa Moja ya Mashambulizi ya Kijinsia ya Jimbo la Michigan**
855-VOICES4; (855-864-2374)
au Ujumbe (866) 238-1454
na TTY (517) 381-8470

**Sparrow Sexual Assault Nurse Examiner (SANE)**
(517) 364-3931

**End Violent Encounters (EVE)**
(517) 372-5572

**The Firecracker Foundation**
517-742-7224

**Laini ya Moja kwa moja ya Kitaifa ya mzozo wa Kinyumbani**
1 (800) 799- 7233

## HUDUMA ZA USHAURI

**Carefree Medical and Behavioral**
(517) 887-5922

**Community Mental Health**
(517) 346-8318

**Child and Family Charities**
(517) 882-4000

**Ele's Place for Grieving Children**
(517) 482-1315

## KUZUIA MIZOZO NA KUJITOA UHAI

**Community Mental Health/ES**
(517) 346-8460

**crisistextline.org**
Tuma ujumbe wa HOME kwa 741741

**The Trevor Project LGBTQIA+**
1 (866) 488-7386 AU
Tuma ujumbe wa START kwa 678678

**suicidepreventionlifeline.org**
Piga simu kwa 988
au Sogoa Mtandaoni

## MATUMIZI MABAYA YA DAWA ZA KULEVYA NA POMBE

**Al-anon and Alateen**
(517) 484-1977
au tembelea www.al-anon.org

**Cristo Rey Counseling Services**
(517) 372-4700

**Child and Family Charities**
(517) 882-4000

**SAMHSA Referral for Services**
1 (800) 662-4357

## HUDUMA ZA AFYA

**Carefree Dental Clinic**
1100 W. Saginaw St. Suite 6A
(517) 272-5053

**Central Michigan Information**
All Community Resources
211

**Planned Parenthood**
Frandor
(517) 351-0550

**Carefree Medical Clinic**
1100 W. Saginaw St. Suite 5
(517) 887-5922

**Ingham County Health Department**
5303 South Cedar Street
(517) 887-4311 or visit hd.ingham.org

**Willow Health Center**
306 W. Willow Street
(517) 702-3500

## HUDUMA ZA WALIOTOROKA MAKWAO/WASIOKUWA NA MAKAO

**Gateway Youth Services**
1 (877) 833-3689

**National Runaway Safeline**
1(800)786-2929 au sogoa mtandaoni kwenye 1800runaway.org

# Matarajio

## Uraia

Bodi ya Elimu ya Lansing School District inatarajia wanafunzi kuwa na mienendo inayolingana na viwango vyao vya kukua, ukomavu na uwezo dhahiri kwa kuzingatia haki na masilahi ya wanafunzi, wafanyakazi wa shule, watu wa kujitolea na wakandarasi wengine.

## Kanuni za Uraia wa Shule

Mwongozo huu unanuia kuhakikisha kwamba kanuni zifuatazo za uraia zinafuatwa:

1. Wanafunzi watahudhuria shule kila siku, kwa wakati unaofaa na wakiwa wamejiandaa kusoma
2. Wanafunzi wataonyesha adabu, ungwana, na heshima kwa wanafunzi na watu wazima wengine
3. Wanafunzi watatenda kwa njia ambayo inaangazia kujivunia wenyewe, familia yao, na shule yao
4. Wanafunzi wataheshimu dhana, imani, na tamaduni za watu wengine kwa uwazi wa fikra na heshima
5. Wanafunzi watatumia lugha au ishara zinazofaa na za heshima wakati wanaongea na wanafunzi na watu wazima wengine
6. Wanafunzi watashirikiana, watakuwa makini, na wa msaada darasani na ukumbini
7. Wanafunzi watasaidia kudumisha mazingira ambayo ni salama, mema na yenye matokeo ya shule
8. Wanafunzi watajitambulisha wenyewe kwa wafanyakazi wa shule wakiombwa

## Chanjo Zinazotakikana ili Kujiunga na Shule katika Michigan

| | Wanachekechea wote na wanafunzi wa umri wa miaka 4-6 waliohamia hapa | Wanafunzi wote wa Gredi ya 7 na wenye umri wa miaka 7-18 waliohamia hapa |
|---|---|---|
| **Diphtheria, Pepopunda, Kifaduro (DTP, DTaP, Tdap)** | Dozi 4 za DTP au DTaP Ni lazima dozi 1 ifanywe katika umri wa miaka 4 au zaidi | Dozi 4 za diptheria na pepopunda au dozi 3 kama ya kwanza ilifanywa akiwa na umri wa mwaka 1 au zaidi<br><br>Dozi 1 ya Tdap akiwa na miaka 11 au zaidi akishajiunga na gredi ya 7 au juu |
| **Polio** | Dozi 4 (dozi 3 kama ya 3 ilifanywa akiwa na miaka 4 au zaidi) | |
| **Surua, Matumbwitumbwi, Rubella (MMR)*** | Dozi 2 akiwa na angalau miezi 12 | |
| **Hepatitis B*** | Dozi 3 | |
| **Meningococcal Conjugate (MenACWY)** | Hamna | Dozi 1 akiwa na umri wa miaka 11 au zaidi akishajiunga na gredi ya 7 au juu |
| **Varicella (Tetekuwanga)*** | Dozi 2 akiwa na umri wa miezi 12 au zaidi, kingamwili ya maabara ya sasa (current lab immunity), au historia ya ugonjwa wa varicella | |

*Iwapo mtoto hajapokea chanjo hizi, rekodi ya kingamwili inatakikana.

**Chanzo:** https://www.michigan.gov/-/media/Project/Websites/mdhhs/Folder2/Folder18/Folder1/Folder118/School_Req_for_Parents.pdf?rev=ce1a8f1ee9454802858071afe83dd2a0

## Nafasi Sawa ya Elimu

Ni sera ya Wilaya hii kutoa nafasi sawa ya elimu kwa wanafunzi wote.

## Kushiriki kwa Wazazi

Kama mzazi au mlezi, kushiriki kwako katika elimu ya mtoto wako kunaweza:


1. Kumsaidia mtoto wako kufikia elimu ya hali ya juu
2. Kuongezea kuridhika kwako na shule
3. Kuongezea ari ya mwalimu

Mtazamo mzuri wa familia na walimu huchangia katika ufanisi wa kielimu wa mtoto wako!

## Haki na Majukumu ya Wazazi na Wanafunzi

1. Kanuni na taratibu za shule zimebuniwa kuruhusu kila mwanafunzi kupata elimu salama, nadhifu na inayofaa. Wanafunzi wanaweza kutarajia haki zao za uhuru wa kujieleza na kukutanika na kutendewa kwa haki ilimradi wanaheshimu haki hizo za wanafunzi na wafanyakazi wao wenza. Wanafunzi watatarajiwa kufuata maagizo ya walimu na kutii kanuni zote za shule. Taratibu za nidhamu zimetengenezwa ili kuhakikisha mchakato wa kisheria (usikilizaji wa haki) kabla ya mwanafunzi kuondolewa kwa sababu ya tabia yake.

2. Wazazi wana haki ya kujua jinsi mtoto wao anafanikiwa shuleni na kupewa maelezo ya mara kwa mara na yakihitajika, wakati hoja yoyote inapoibuka. Wakati mwingi itakuwa ni wajibu wa mwanafunzi kuwasilisha maelezo hayo. Ikihitajika, barua au uwasilishaji wa mkono unaweza kutumika ili kuhakikisha mawasiliano. Wazazi wanahimizwa kudumisha mawasiliano kati ya walimu wa watoto wao na wafanyakazi kwa kufahamisha wafanyakazi kuhusu mapendekezo au hoja ambazo zinaweza kusaidia mtoto wao kukamilisha malengo yake ya elimu.



### Jihusishe – Jiunge na Baraza la Ushauri la Wazazi/Jumuiya (PCAC, Parent/Community Advisory Council)!

Toa maoni na ufahamishwe kuhusu mambo yote ya Lansing School District. Jiunge na wafanyakazi wa wilaya na wazazi kuanzia 6-8:00pm Jumatano ya mwisho ya kila mwezi!

**Mikutano hufanyika katika:**
4200 Wainwright Avenue
Lansing, MI 48911

**Una Maswali?**
Piga simu kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule (Office of School Culture)
(517) 755-2800




**Darin Walter**
*Mratibu wa Title IX*
darin.walter@lansingschools.net
517-755-2037

**Erin Miracle**
*Afisa wa Kufuatilia Title IX*
erin miracle@lansingschools.net
517-755-2010

Lansing School District
519 West Kalamazoo
Lansing, MI 48933

*Bodi imewateua watu walio hapa juu ili kuhudumu kama "Mratibu wa Title IX" na "Afisa wa Ufuatiliaji wa Title IX" katika Wilaya. Wanaorejelewa hapa kama "Maafisa wa Utekelezaji."*

3. Lazima wanafunzi wafike shuleni kwa wakati unaofaa, wakiwa tayari kusoma na kushiriki katika mpango wa elimu. Ikiwa, kwa sababu yoyote ile, hii haiwezekani, mwanafunzi anapaswa kutafuta msaada kutoka kwa mwalimu mkuu, mwalimu, au karani wa jamii ya shule.
   i. Wanafunzi watu wazima (wenye umri wa miaka 18 au zaidi) lazima wafuate kanuni zote za shule.
   ii. Ikiwa wanaishi nyumbani, wanafunzi wote watu wazima wanapaswa kujumuisha wazazi wao katika mpango wao wa elimu.

## Haki

1. Kuelimishwa katika mazingira mazuri na salama
2. Kushiriki katika mchakato wa elimu katika mazingira yasiyokuwa na hofu, unyanyasaji, vitisho, usumbufu na uhasama
3. Kutarajia kwamba kanuni za shule zitatekelezwa kwa njia thabiti, ya haki na inayofaa
4. Kupata uwezo wa kukagua rekodi za wanafunzi (Wanafunzi chini ya umri wa miaka 18 wanaweza kushiriki katika mkutano kama huo; wale walio na umri wa miaka 18 na zaidi wanaweza kuomba mkutano bila wazazi wao kuwepo)
5. Kutarajia kwamba wafanyakazi wa shule watachunguza ripoti za ukiukaji wowote wa haki za wanafunzi na wazazi na kujibu kwa wakati
6. Kurudia kazi zote zilizokosekana kwa sababu ya kutokuwepo au kuondoshwa
7. Kuomba mkutano wa elimu na wafanyakazi wa shule
8. Kuwasilisha malalamiko, matukio, matatizo, malalamiko, au maombi ya rufaa kwa mwalimu mkuu na kupokea majibu ya kwanza ndani ya siku tatu (3) za shule baada ya mwalimu mkuu kupokea
9. Kupokea misaada kwa matatizo na masuala ya afya, hasa kwa wanafunzi wenye hali sugu za afya (k.m. dawa, uchunguzi wa afya, na hatua za kuingia kali)

Ni sera ya Bodi ya Elimu kudumisha mazingira ya elimu ambayo hayana aina yoyote ya unyanyasaji kinyume na sheria, ikiwemo unyanyasaji wa kingono. Wilaya haitakubali uyanyasaji wa kingono au aina nyingine za unyanyasaji kinyume cha sheria. Ahadi hii inalenga huduma zote za School District,

mipango na shughuli zote za elimu na zisizo za elimu. Wanafunzi wote, wasimamizi, walimu, wafanyakazi, na wahudumu wengine wote wa shule wanashiriki wajibu wa kuepusha, kutohimiza, na kuripoti aina yoyote ya unyanyasaji kinyume cha sheria. Sera hii inatumika kwa tabia iliyo kinyume cha sheria ambayo inafanyika wakati wa shughuli ya elimu au ya baada ya masomo inayodhaminiwa na Bodi kwenye majengo ya shule, basi la shule au eneo lingine ikiwa tabia kama hiyo inafanyika wakati wa tukio au shughuli inayodhaminiwa na Bodi.

Mtu yeyote anayetaka kuripoti ukiukaji wa sera ya unyanyasaji anapaswa kuwasiliana na: Maafisa wa Kutekeleza Sera ya Kuzuia Unyanyasaji (wameorodheshwa hapa juu).

Lansing School District, inapofaa, itatoa msaada wa ziada kwa wanafunzi walioripotiwa kuwa waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia au mashambulizi ya kingono. Msaada huu unajumuisha (lakini haujakomea kwa) amri ya kutokutana au mabadiliko katika ratiba ya mwanafunzi ili kumlinda mwanafunzi. Isitoshe, wilaya itatoa msaada wa ushauri, msaada na rasilimali za ziada za elimu kwa wanafunzi ambao wamepitia au waliohusika katika unyanyasaji wa kingono na/au kwa mnyanyasaji.

Mfanyakazi anayeshindwa kuripoti unyanyasaji unaoshukiwa kwa mwalimu wake mkuu, msimamizi, au Maafisa wa Utiifu wa Wilaya ataadhibiwa mara moja. Adhabu kama hiyo inaweza kujumuisha, ikiwa hali inaruhusu, kuondoshwa kwa muda au kufukuzwa kwa mfanyakazi huyo.

Wanafunzi au wafanyakazi wanaolipiza kisasi dhidi ya watu wanaoripoti unyanyasaji wa kingono wataadhibiwa mara moja. Ikiwa hali inaruhusu, nidhamu kama hiyo inaweza kujumuisha kuondoshwa kwa muda au kufukuzwa kwa mwanafunzi, au kuondoshwa kwa muda au kufukuzwa kwa mfanyakazi.

## Majukumu

1. Kujiheshimu binafsi na wengine, na hata pia mali ya wilaya na jamii
2. Kuheshimu kanuni za shule na kushiriki katika kesi za nidhamu
3. Kupanga miadi ili kupitia rekodi kwa wakati unaokubalika na wote
4. Kuripoti ukiukaji wowote wa haki za wanafunzi/wazazi kwa wafanyakazi wa shule
5. Kurudia kazi inayotokana na kutokuwepo au kuondoshwa kwa muda

# Na majukumu yako



## Usaidizi wa Afya ya Kiakili

Lansing School District inaupa kipaumbele utunzaji wa Mtoto kwa Ujumla (Whole Child) ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya jumla ya wanafunzi wake yanabainishwa na kutimizwa. Ahadi hii inajumuisha ufikiaji wa jumla kwa huduma za afya ya akili bila malipo.

Unahimizwa kutumia ushirikiano wetu na Care Solace* ili kupokea huduma za rufaa za tiba za faragha. Care Solace inapatikana saa zote – ikiwemo usiku, wikendi, na sikukuu – katika zaidi ya lugha 200 ili kufafanua chaguo ulizo nazo na kupanga huduma.

**Wasiliana na Care Solace**
Piga simu au tuma SMS kwa (888)515-0595
www.caresolace.com/site/lansing

**Una Maswali?**
Ofisi ya Utamaduni wa Shule
(517) 755-2800

* Care Solace haitoi huduma za afya ya akili. Kwa hali za dharura za afya, tafuta usaidizi wa matibabu katika chumba cha karibu cha dharura, piga simu kwa 911 au kwa Timu ya Kitaifa ya Kuzuia Matukio ya Kujiua (National Suicide Prevention Lifeline) kupitia 988.

**Tunakushauri kuvaa nguo za kijani kila Jumatatu ili kuunga mkono Uhamasisho wa Afya ya Kiakili!**

6. Kushiriki katika mkutano wa elimu na wafanyakazi wa shule
7. Kufuatilia malalamiko kupitia taratibu zilizowekwa
8. Kufuata maagizo kuhusu wakati wa kumweka mtoto mgonjwa nyumbani
9. Kutoa maelezo ya dawa kwa ofisi za shule (k.m. muuguzi wa shule) ikiwemo hati za matibabu zinazohitajika kwa mabadiliko hayo. (Ni muhimu kwamba fomu ya shule iliyokamilisha na kutiwa saini ya Idhini ya Dawa kwa dawa zinazoagizwa na daktari au fomu ya dawa iliyokamilishwa na kutiwa saini ya dawa za Kwenye Kaunta ipewe shule).
10. Kutoa nambari za simu za dharura ambazo zinafanya kazi na mawasiliano ya kutegemewa ya dharura kwa hali za dharura za wanafunzi.

## Ustawi wa Wanafunzi

1. Usalama wa wanafunzi ni wajibu wa wafanyakazi. Wafanyakazi wote wanahitajika kufahamu taratibu za dharura kama vile moto, kusitishwa kwa shughuli za kawaida, mafunzo ya kimbunga na taratibu za kuripoti dharura. Iwapo mwanafunzi atafahamu kuhusu hali au tukio lolote la hatari, lazima aarifu mfanyakazi yeyote mara moja.
2. Sheria ya jimbo inahitaji kwamba ni lazima wanafunzi wote wakamilishe kadi ya matibabu ya dharura, iliyotiwa saini na mzazi au mlezi, na kujazwa katika ofisi ya shule. Mzazi anaweza kuondolewa shuleni hadi hitaji hili litimizwe.
3. Wanafunzi walio na mahitaji maalum ya huduma ya afya wanapaswa kuwasilisha ilani iliyoandikwa kuhusu mahitaji kama hayo pamoja na hati zinazofaa zinazotolewa na daktari, kwa ofisi ya shule.

## Ripoti ya Lazima ya Unyanyasaji au Utelekezaji wa Watoto

Lansing School District inatii Sheria ya Michigan ya Ulinzi wa Watoto inayowahitaji watu fulani kuripoti tuhuma zao za kutelekezwa au kunyanyaswa kwenye Huduma za Ulinzi wa Watoto. Tafadhali angalia tovuti ya Sheria ya Michigan na Sheria ya Ulinzi wa Watoto – DHS Pub-3 ili upate maelezo Zaidi.

## Magonjwa na Majeraha

1. Lazima majeraha yote yaripotiwe kwa mwalimu na au ofisi. Ikiwa majeraha ni madogo, mwanafunzi atatibiwa na kurudi darasani. Ikiwa matibabu yanahitajika, ofisi itafuata taratibu za dharura za shule.

2. Mwanafunzi ambaye atakuwa mgonjwa wakati wa siku ya shule anapaswa kuomba ruhusa ya kwenda ofisini. Mtu mzima anayefaa katika ofisi ataamua kama mwanafunzi anapaswa kusalia shuleni au kwenda nyumbani. Hakuna mwanafunzi ataruhusiwa kutoka shuleni bila ruhusa inayofaa ya mzazi.

## Sera na Sheria za Mahudhurio

Bodi ya Elimu inaamini kwamba mahudhurio ni jambo muhimu katika mafanikio ya wanafunzi na kwamba kutokuwepo shuleni kunawakilisha hasara ya elimu kwa mwanafunzi. Mitindo ya mara kwa mara na ya wakati upasao ya mahudhurio itatarajiwa kwa kila mwanafunzi aliyesajilia katika Wilaya ya Shule za Lansing.

Ijapokuwa inatambuliwa kwamba kutokuwepo shuleni ni muhimu chini ya hali nyingine, kila juhudi inapaswa kuchukuliwa na wanafunzi, wazazi/walezi, walimu na wasimamizi ili kupunguza kabisa kutokuwepo na kuchelewa.

Mahudhurio ya wanafunzi ni wajibu wa mzazi/mlezi na mwanafunzi. Ili wazazi/walezi watimize wajibu wao, lazima shule iwafahamishe kuhusu mitindo ya kutokuwepo na mahudhurio ya wanafunzi.

Mfumo unaotosha na kamili wa rekodi za mahudhurio unapaswa kudumishwa kwa kila mwanafunzi. Kila mwalimu anawajibika kutoa ripoti sahihi za mahudhurio ya kila siku katika darasa lake. Mwalimu mkuu atawajibika kuhakikisha usahihi wa rekodi zote za mahudhurio za shule yake.

Kutohudhuria masomo, hata kule kunakoidhinishwa na mzazi/mlezi, ambako kunazidi kupita kiasi na/au kunatatiza mpango wa elimu wa mwanafunzi, kutachunguzwa na mhudumu wa wilaya ya shule.

Wanafunzi wote watakuwa na nafasi ya kurudia kazi za shule zilizokosekana kwa sababu ya kutokuwepo. Hata hivyo, itakuwa ni wajibu wa mwanafunzi kupata kazi hizo na kuzirejesha ndani ya muda uliokubaliwa na kila mwalimu.

Ni azimio la Mpango wa Kuboresha Mahudhurio ya Lansing School District kuendeleza ufanisi wa wanafunzi kwa kukuza utamaduni wa mahudhurio mazuri, kukuza mabadiliko ya mtazamo na kutoa nafasi sawa za masomo kwa kuongezea mahudhurio ya wanafunzi.

### Tunaamini

1. Katika kutambua na kupunguza vikwazo ili kuziba mianya ya usawa.
2. Katika kukuza mtazamo wa kukua wa wafanyakazi, wanafunzi na familia.
3. Katika kukuza mahudhurio ya siku nzima kama kipaumbele.
4. Katika hitaji la kushirikiana na familia na washiriki wa jamii.
5. Katika kuunda na kudumisha tabia thabiti za mahudhurio mapema na katika maisha yote ya mwanafunzi.
6. Katika kanuni zinazofaa tamaduni ambazo zinaunga mkono mahudhurio mema.
7. Katika kukusanya na kutumia data mbalimbali zinazoweza kuchukuliwa hatua ili kutumia mbinu ya safu ya kuboresha mahudhurio.
8. Katika matokeo ambayo mahudhurio mema ya wafanyakazi inayo kwa mahudhurio ya wanafunzi.
9. Katika kuhimiza na kusheherekea mahudhurio yaliyoimarika.

## Mahudhurio na Kutokuwepo kwa Wanafunzi

Wanafunzi wanatarajiwa kufika shuleni kabla ya shule kuanza kila siku. Umuhimu wa kuhudhuria mara kwa mara ni somo muhimu la kufunzwa shuleni. Masomo yanaendelea kila siku darasani. Matukio haya ya kusoma hayawezi kurudufiwa. Wakati mwanafunzi anakosa shule, anakosa sehemu ya thamani ya elimu yake.

Mwanafunzi wa K-12 anachukuliwa kuwa hayupo anapokosa kipindi kizima cha darasa. Mwanafunzi amechelewa wakati anakosa hadi dakika 15 za kipindi cha darasa. Mwanafunzi anachukuliwa Amewasili Amechelewa (AL) wakati anapowasili dakika 15 baada ya kuanza kwa kipindi cha darasa. Wanafunzi wanaoondoka darasani kabla ya muda uliopangwa wa tamati na hawarudi watachukuliwa Wametoka Mapema (LE).

### Je, Mtoto Wangu Anaruhusa ya Kutokuwepo?

Kutohudhuria kumeruhusiwa ikiwa arifa itapokewa na shule ndani ya siku kumi (10) za shule baada ya kutohudhuria huko, ambako kunatokana na sababu moja kati ya zifuatazo:

- Ruhusa ya Mzazi kwa sababu ya Ugonjwa (hadi na kujumuisha 10 kwa mwaka) Kutokuwepo baada ya mara 10 kwa mwaka, hakutaruhusiwa isipokuwa kuwa na udhuru wa matibabu (wa daktari)
- Mazishi
- Sababu Zinazohusiana na Shule (kufukuzwa kwa muda, basi za kuchelewa, ziara za nyanjani)
- Kuhudhuria Mahakama/Kesi
- Kufungwa gerezani
- Ruhusa ya Kimatibabu (Daktari)
- Maadhimisho ya Kidini

## Taratibu za Gredi ya K-6

1. Wazazi/walezi wa kisheria watawajibika kuwasiliana na ofisi ya shule ikiwa mwanafunzi hatakuwepo. Matokeo ya mawasiliano hayo yatawekwa kwenye rekodi rasmi ya mahudhurio.
2. Mhudumu wa shule atapiga simu nyumbani ikiwa mzazi/mlezi wa kisheria hajapiga simu kuthibitisha sababu ya kutokuwepo kwa mwanafunzi. Matokeo ya mawasiliano hayo yatawekwa kwenye rekodi rasmi ya mahudhurio.
3. Wakati wanafunzi wanaporejea baada ya kutokuwepo, wanapaswa kuleta barua iliyoandikwa kutoka kwa mzazi/mlezi wa kisheria inayoelezea sababu ya kutokuwepo.
4. Wafanyakazi wa shule watawasiliana na mzazi/mlezi wa kisheria wakati mwanafunzi amefikisha siku tano (5) kamili (siku kumi (10) nusu) za kutokuwepo.
5. Wanafunzi waliofikisha siku nane (8) kamili (siku kumi na sita (16) nusu) za kutokuwepo wanaweza kuelekezwa kwa Mtaalamu wa Mahudhurio wa wilaya.
6. Wakati wanafunzi wanapozidisha siku kumi (10) kamili za kutokuwepo wakiwa na ruhusa ya mzazi (ugonjwa au ombi la familia), barua iliyoandikwa kutoka kwa daktari wa mwanafunzi itahitajika. Ni lazima taarifa hiyo ijumuishe sababu ya kutohudhuria, idadi ya siku ambazo mwanafunzi hatahudhuria, tarehe za kutohudhuria na saini ya daktari.
7. Kabla ya rufaa kufanywa kwa Mtaalamu wa Mahudhurio, barua itatumwa kwa shule ili kuarifu mzazi/mlezi wa kisheria kuhusu matatizo ya mahudhurio.
8. Ikiwa juhudi zote hapo juu zitashindwa kutatua tatizo la mahudhurio, Mtaalamu wa Mahudhurio ataendelea na hatua ya kisheria au nyingine inayofaa dhidi ya mzazi.

## Taratibu za Gredi za 7- 12

Kutohudhuria kumeruhusiwa ikiwa taarifa itapokelewa na shule ndani ya siku kumi (10) za shule baada ya kutohudhuria huko, ambako kunatokana na mojawapo ya sababu iliyoorodheshwa kwenye ukurasa wa 13.

1. Wazazi/walezi wa kisheria watawajibika kuwasiliana na ofisi ya shule ikiwa mwanafunzi hatakuwepo. Matokeo ya mawasiliano hayo yatawekwa kwenye rekodi rasmi ya mahudhurio.

2. Wakati wanafunzi wanapozidisha siku kumi (10) kamili za kutokuwepo wakiwa na ruhusa ya mzazi (ugonjwa au ombi la familia), barua iliyoandikwa kutoka kwa daktari wa mwanafunzi itahitajika ili kuruhusu kutokuwepo zaidi. Lazima taarifa hiyo ijumuishe sababu ya kutokuwepo, idadi ya siku ambazo mwanafunzi hatakuwepo, tarehe za kutokuwepo na saini ya daktari.

3. Mwalimu ataarifu usimamizi au uwakilishi wa shule wakati mwanafunzi anapokosa kwenda shuleni mara kumi (10) (na au bila ruhusa) au wakati mitindo isiyo ya kawaida ya kutohudhuria inapofanyika katika kipindi cha darasa katika muhula, na shule itamwarifu mzazi (kupitia barua pepe, simu au ana kwa ana).

4. Ikiwa juhudi zote hapo juu zitashindwa kutatua tatizo la mahudhurio na mwanafunzi yuko chini ya umri wa miaka 18, Mtaalamu wa Mahudhurio anaweza kuendelea na hatua ya kisheria au nyingine inayofaa dhidi kwa mwanafunzi na ya mzazi au mlezi. Ikiwa mwanafunzi yuko kati ya umri wa miaka 16 na 18, wazazi wanaweza kumwondoa mwanafunzi shuleni kwa kutia saini fomu ya Ridhaa ya Kumwondoa Mwanafunzi Shuleni katika uwepo wa msimamizi wa shule. Fomu hii inapatikana katika kila shule ya upili.

## Huduma za Nyumbani

Ikiwa mwanafunzi wako amegunduliwa na daktari wake kuwa ana hali ya matibabu inayomzuia kwenda shuleni (siku 5 au zaidi), unaweza kustahiki huduma za nyumbani.

### Huduma za Nyumbani ni nini?

Wilaya ya Shule za Lansing inatoa huduma za nyumbani kwa wanafunzi wale wanaopokea matibabu ambayo yanawazuia kuhudhuria shule kama kawaida. Kwa kutumia kazi, vitabu, na/au nyenzo za mtandaoni zinazotolewa na darasa la shule, walimu waliohitimu wa nyumbani wanatoa msaada wa mafunzo katika nyumba ya mwanafunzi.

### Mahitaji ya Kustahiki:

Ili kustahiki huduma za nyumbani, lazima mtoto wako:

- Awe amepata hati ya uchunguzi wa matibabu ambayo unamzuia kuhudhuria muda wote
- Awe na fomu ya rufaa ya daktari kutoka kwa mtaalamu aliyethibitishwa wa matibabu (M.D., D.O., au a Msaidizi Aliyethibitishwa wa Daktari)
- Awe hajakuwepo shuleni kwa sababu za kimatibabu kwa siku zinazozidi tano (5) mtawalia
- Awe amesajiliwa katika Wilaya ya Shule za Lansing

### Nguvu ya Ushirikiano

Walimu wetu wa nyumbani hushirikiana na mwalimu wa darasa wa mtoto wako ili kumpa mwanafunzi wako nyenzo na kazi zinazohitajika. Mwalimu wa darasa wa mtoto wako atasalia kuwa mwalimu kwenye rekodi ya mtoto wako.

### Walimu wa Nyumbani:

- Watapanga huduma na mzazi
- Watatoa msaada wa mafunzo kwa kumpa mwanafunzi wa nyumbani kazi, vitabu, na rasilimali za mwalimu
- Watarejesha kazi iliyokamilishwa shuleni
- Watahudumu kama wapatanishi kati ya familia yako na shule ya mtoto wako

### Ninawezaje Kumwandikisha Mtoto Wangu?

1. Omba na uwasilishe fomu ya rufaa ya mwanafunzi kwa shule yako. Kisha mshauri au msimamizi wa shule atakamilisha fomu ya rufaa na kuwasilisha zote kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule (OSC).

2. Kisha mshauri wa shuleni atapata fomu ya rufaa ya daktari na kuwasilisha fomu zote tatu kwa Pupil Accounting and Central Enrollment Office (PACE) kwa idhini ya mwisho. Utaarifiwa ndani ya wiki moja ukishawasilisha ikiwa/wakati huduma za nyumbani zitatolewa.

Unamjua mwanafunzi wa LSD ambaye anaishi kwenye nyumba ya wengine au hana makao?

**Mpango wa F.O.R.T. unaweza kusaidia!**

FORT
families overcoming rough times

**Tuma ombi la faragha leo!**

Bado hujajiunga na familia?
Jisajili Sasa!
www.enrollinlansing.com

## Vijana na Watoto Wasio na Makao

Sheria ya McKinney- Vento ya Elimu ya Wasio na Makao inalinda haki za elimu kwa watoto na vijana wasio na makao. Lengo kuu ni uthabiti wa elimu.

Sheria hiyo inabainisha wanafunzi wasio na makao kuwa:

1. Wasio na mahali pamoja wanapoenda kupumzika usiku kila mara;
2. Wanaishi na wengine, wanaishi katika moteli, hoteli, maegesho ya magari ya mizigo au maeneo ya kupiga kambi kutokana na kukosa makazi bora; wanaishi katika vibanda vya dharura au vya kuhamisha;
3. Wana makazi ya usiku ambayo ni sehemu ya umma au ya faragha ambayo hayajaundwa au kwa kawaida hayatumiwi kama sehemu ya kulala mara kwa mara na binadamu;
4. Wanaishi katika magari, bustani, maeneo ya umma, majengo yaliyotelekezwa, majumba ya kiwango cha chini, vituo vya basi au treni, au maeneo kama hayo;
5. Wanahama kila mara na wanaishi katika hali zilizobainishwa katika hoja za 2-4 hapo juu.

Wanafunzi wasio na makao wana haki fulani za elimu na wanaweza: kujiandikisha bila kuchelewa shuleni (shule ya karibu au ya asili) bila uthibitisho wa makazi au anwani ya kudumu, kupokea chanjo, rekodi za shule, au hati nyingine au wakati wanatafuta hati; kuchagua kati ya shule ya karibu na wanakoishi au shule waliohudhuria kabla ya kukosa makazi, wakati mzazi au mlezi anaomba na ikibainishwa na wilaya kuwa inawezekana na ni chaguo bora kwa maslahi ya mwanafunzi; kuhudhuria shule na kushiriki katika mipango ya shule pamoja na watoto ambao wana makazi; na kupokea huduma zote za shule zinazopatikana kwa wanafunzi wengine, ikiwa ni pamoja na huduma za usafiri, elimu maalum panapohiajika, na huduma nyingine za usaidizi (chakula, makazi, mavazi nk).

Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma za wasio na makao,
ikiwa ni pamoja na kukagua ustahiki na kujiandikisha, wasiliana na

**Families Overcoming Rough Times (FORT) Simu (517) 755.2813**

## Haki za Wanafunzi za Kujieleza

Shule inatambua haki za wanafunzi za kujieleza. Na haki za kujieleza kuna wajibu wa kuzitekeleza kwa njia inayofaa. Wanafunzi wanaweza kusambaza au kuonyesha, kwa wakati unaofaa, nyenzo zilizoandikwa na maombi yasiyofadhiliwa na yasiyokuwa ya kibiashara; vitufe, beji, au nembo nyingine; mavazi, nembo, na mabango; na nyenzo za sauti na video. Lazima vitu vyote vifuate maagizo ya shule:

1. Nyenzo haiwezi kuonyeshwa ikiwa:
   - **i.** ni chafu kwa watoto, ni ya kukashifu, si sahihi, au ina matusi
   - **ii.** inatanganza bidhaa au huduma zozote zisizoruhusiwa kwa watoto kisheria
   - **iii.** inalenga kutusi au kunyanyasa
   - **iv.** inalenga kuchochea vita au inasababisha uwezekano wa kutatiza shule au tukio la shule
   - **v.** inawakilisha uwezekano wazi na dhahiri kwamba, aidha kwa sababu ya maudhui yake au njia ya kusambaza au kuonyesha, inaweza kutatiza shule au shughuli za shule, ukiukaji wa sheria za shule, au kusababisha kitendo ambacho ni kinyume cha sheria
2. Huenda nyenzo zisionyeshwe au kusambazwa wakati wa vipindi vya darasa au nyakati kati ya madarasa. Ruhusa inaweza kupeanwa ya kuonyesha au kusambaza wakati wa vipindi vya chakula cha mchana na baada ya shule katika maeneo yaliyoteuliwa, ilimradi milango ya kutoka isiwe imezibwa na kuna njia sahihi na ya kutoka shuleni.

Wanafunzi ambao hawana uhakika kama nyenzo wanazotaka kuonyesha zinatimiza maagizo ya shule au la wanaweza kuziwakilisha kwa mwalimu mkuu wa shule saa ishirini na nne (24) kabla ya kuonyesha.

## Hoja, Mapendekezo na Malalamiko ya Wanafunzi

Shule iko hapa kwa manufaa ya wanafunzi. Wafanyakazi wako hapa ili kumsaidia kila mwanafunzi katika kuwa mtu mzima anayewajibika. Ikiwa mwanafunzi ana mapendekezo ambayo yanaweza kuboresha shule, anapaswa kuhisi huru kuyatoa. Mapendekezo yaliyoandikwa yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja kwa mwalimu mkuu au kwa chama cha wanafunzi.

Wakati hoja au malalamiko yanapotokea, njia bora ya kutatua tatizo hilo ni kupitia mawasiliano. Hakuna mwanafunzi atanyanyaswa na mfanyakazi yeyote au kuwa na hofu ya kulipizwa kisasi kwa kuelezea vizuri wasiwasi halali. Mapendekezo, hoja, au malalamiko yoyote yanaweza kuelekezwa kwa mwalimu mkuu au kwa chama cha wanafunzi.






### Barakoa za Uso

Iwapo mwanafunzi atachagua kuvaa barakoa, masharti yafuatayo yatatumika: Barakoa zinazofunika uso mzima, zinazofunika shingo na sehemu ya chini ya mdomo, au bandana haziruhusiwi. Lazima barakoa zifuate mwongozo wa CDC na muundo unaopendekezwa.

* Mwalimu mkuu atakuwa na mamlaka ya kuruhusu uvaaji wa koti.

## Kijitabu cha Mavazi cha Wilaya Nzima

Nguo zinazovaliwa shuleni zinapaswa kuwa nzuri na safi. Ili kudumisha mazingira mazuri, salama na yenye mpangilio, lazima viatu vivaliwe. Viatu ambavyo vinaweza kusababisha hatari kwa usalama wa wanafunzi, kama vile viatu vyenye magurudumu, vimepigwa marufuku. Viatu kama vile koshi na vyenye visigino havipendekezwi, lakini vinaweza kuvaliwa kulingana na uamuzi wa mzazi. Mavazi ya nje kama vile koti, kofia au vilemba (isipokuwa kwa sababu za kidini au kimatibabu) jaketi, na miwani isiyoagizwa na daktari hazitavaliwa katika majengo ya shule.

Haturuhusu mavazi ambayo yanaonyesha uchi, yenye matusi, au yanayoonyesha lugha chafu, shughuli au vitu visivyo halali (k.m pombe, dawa za kulevya, tumbaku, n.k.), maneno au picha za kukera, au nembo, alama au ujumbe wa magenge. Wanafunzi hawapaswi kuvaa minyororo mikubwa au shanga za shingoni. Beji au mapambo yanayoonyesha ujumbe wa au kutambulisha mashirika ambayo yanajulikana kudhulumu watu kulingana na mbari, kabila, nchi, rangi, ngono, mkao wa ngono, umri, dini, au ulemavu wa akili au mwili, zimepigwa marufuku.

Mavazi yasiyokubaliwa yatajumuisha, lakini hayajakomea kwa, vitanzi, mavazi yanayoonyesha tumbo au kifua, blausi fupi, au shati za kuonyesha misuli, (isipokuwa kama zimevaliwa ndani ya T-shati), blausi za kamba, nguo za kulala, na mifuto au suruali chini ya kiuno ili kufichua suruali za ndani au ngozi. Suruali/mifuto iliyoning'inia haziruhusiwi. Lazima suruali zitoshee kiuno bila kushikwa kwa mikono. Mavazi yanapaswa kufunika mwanafunzi kikamilifu upande wa nyuma akiwa ameinama.

Wanafunzi, pamoja na wazazi wao, wana wajibu wa kuvaa na kujipamba wenyewe kwa njia inayofaa shuleni. Hata hivyo, fasiri ya mavazi inabainishwa na usimamizi wa shule kwa njia isiyobadilika, ya haki na ya kueleweka:

## Kijitabu cha Wanafunzi cha Shughuli za Baada ya Masomo

Wanafunzi wa Lansing na wageni wao wanaohudhuria matukio yanayohusiana na shule watasimamiwa na Mwongozo wa Lansing School District na wanaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu, ikiwemo kuondolewa kwenye timu ikiwa watakiuka Mwongozo huu.

Makocha na wafadhili wanaweza kuweka seti ya ziada ya kanuni kwa washiriki kwa idhini ya mapema kutoka kwa mwalimu mkuu. Ikiwa seti ya kanuni itawekwa, lazima kanuni hizo ziandikwe na kupewa washiriki kabla ya msimu wa shughuli hiyo. Nakala za kanuni zilizotiwa saini na kila mshiriki na mzazi lazima ziwe kwenye faili katika ofisi ya mwalimu mkuu.

## Usambazaji wa Nyenzo Zilizochapishwa

Nyenzo ambazo zimeidhinishwa na mwalimu mkuu tu ndio zinaweza kuchapishwa au kusambazwa.

Mwalimu mkuu au mwakilishi ataweka saa na maeneo mahsusi ya usambazaji wa nyenzo zilizochapishwa na wanafunzi. Nyenzo zote zilizosambazwa lazima ziwe na jina la mtu au shirika linalodhamini na ziashirie mwandishi au mchapishaji.

Mwalimu mkuu au mwakilishi anaweza kuchukua nyenzo zozote ambazo hazijaidhinishwa mapema.

## Kanuni za Matumizi ya Vifaa vya Mawasiliano vya Kielektroniki (ECD)

ECD ni vifaa vyote vya kielektroniki vinavyotumiwa kuwasiliana na vingine na vinajumuisha simu za mkononi, iPad na kompyuta za kibinafsi. Matumizi ya ECD kwa njia isiyoidhinishwa yanaweza kusababisha hatua ya kinidhamu, ikiwemo kunyang'anywa, kulingana na hali ya shughuli iliyopigwa marufuku na/au kama ni kosa la kurudia la mwanafunzi huyo. Usimamizi una haki ya kurekebisha matokeo kama inavyofaa. Lazima ECD zikabidhiwe msimamizi au Afisa wa Usalama wa Umma ikiombwa.

Matumizi yasiyofaa ya ECD yoyote yamepigwa marufuku kabisa. ECD zinaweza kosa "kuwashwa" au kutumiwa katika vyumba vya makabati au vya msalani, iwe hapa au katika wilaya nyingine ya shule ambapo shughuli ya shule au tukio la riadha linafanyika. Kifaa chochote cha aina hii kitachukuliwa na mwanafunzi kuchukuliwa hatua ya kinidhamu.

Wanafunzi wanaomiliki ECD watawajibika kukitunza.

1. Hakuna wakati wowote Wilaya itawajibika kuzuia wizi, upotezaji, uharibifu wa ECD zilizoletwa katika majengo ya shule na/au mabasi. Wanafunzi na wazazi wanahimizwa kuhakikisha kwamba, ikiwa wanafunzi wanamiliki ECD, wanapaswa kuzitunza na kuzilinda.

2. Wakati wowote ule, matumizi ya vifaa vya mawasiliano vya elektroniki, au mitandao ya kijamii kunyanyasa, kutishia au kuunda mazingira mabaya shuleni, au kutatiza mazingira ya masomo kutasababisha hatua ya kinidhamu. Ni pamoja na kunyang'anywa kifaa hadi kufukuzwa kwa muda shuleni.




### Matumizi mabaya ya ECD Yanaweza Kusababisha...

**Kosa la 1** Kifaa kitachukuliwa na kurejeshewa mwanafunzi mwisho wa siku.

**Kosa la 2** Kifaa kitachukuliwa, mzazi/mlezi ataambiwa akujie kifaa mwisho wa siku, na fursa ya ECD kubatilishwa.

**Makosa Yanayofuatilia** Kifaa kitachukuliwa na tutachukua hatua za ziada za kinidhamu hadi kufukuzwa kwa muda shuleni..




# Matumizi ya Teknolojia na Kanuni za Usalama

Matumizi ya teknolojia katika Wilaya ya Shule za Lansing ("wilaya") ni fadhila iliyopewa wanafunzi. Fadhila hiyo ina wajibu wa kutumia teknolojia kwa njia ambayo inalingana na Kijitabu hiki na hata pia sheria na masharti yote husika. Lazima matumizi ya teknolojia yalingane na misheni ya wilaya na yalenge kuboresha mchakato wa elimu pekee. Teknolojia inarejelea, lakini haijakomea kwa, ECD, barua ya sauti, maunzi ya kompyuta, programu na vipembezo, vifaa vya kompyuta vya mkononi, vikokotoo, vifaa vya sayansi, televisheni, barua pepe rasilimali za intraneti na ufikiaji wa intaneti.

## Kanuni za Teknolojia kwa Gredi ya K-6

1. Wanafunzi watatumia vifaa vya elektroniki kwa ruhusa ya mwalimu tu na watafuata maagizo yote ya mwalimu ya matumizi,
2. Wanafunzi hawatampa mtu yeyote kwenye intaneti jina lao, jina la shule, anwani ya nyumbani au nambari ya simu,
3. Ikiwa mwanafunzi atapata maelezo katika ECD ambayo yanafanya mwanafunzi asihisi vizuri, au ambayo anajua ni mabaya, mwanafunzi anapaswa kumweleza mwalimu,
4. Ikiwa mwanafunzi atapata ujumbe ambao sio mzuri au unamfanya ahisi vibaya, mwanafunzi huyo anapaswa kumweleza mwalimu mara moja na ASIJIBU ujumbe huo,
5. Wakati mwanafunzi anatumia ECD, mwanafunzi huyo atakuwa makini sana asivunje au kuharibu sehemu yake yoyote,
6. Mwanafunzi hatasanidi, kupakua, au kutumia programu yoyote ambayo haijaidhinishwa na Idara ya Teknolojia. Hii ni pamoja na, lakini haijakomea kwa programu yoyote iliyopakuliwa kutoka kwa CD, hifadhi au inayopatikana kwenye intaneti.

## Kanuni za Teknolojia kwa Gredi ya 7- 12

1. Mwanafunzi atatumia ECD kwa malengo yaliyoidhinishwa ya elimu pekee,
2. Kwa kutambua kwamba matumizi ya ECD ni fursa, mwanafunzi anakubali kuwajibika kutunza vizuri teknolojia zote ambazo ameidhinishwa,
3. Mwanafunzi ataweka salama akaunti na manenosiri yote aliyopewa na hatashiriki na wanafunzi, wafanyakazi au wageni wengine. Hii ni pamoja na manenosiri ya barua pepe na kufikia mtandao,
4. Mwanafunzi hatawahi kushiriki maelezo ya kibinafsi kwenye Intaneti,
5. Isitoshe, ikiwa mwanafunzi ataombwa maelezo ya kibinafsi au kunyanyaswa kwa njia yoyote ile, anakubali kuripoti mara moja kwa mwalimu au mfanyakazi mwingine,
6. Mwanafunzi hatasanidi, kupakua, au kutumia programu yoyote ambayo haijaidhinishwa na Idara ya Teknolojia. Hii ni pamoja na, lakini haijakomea kwa programu yoyote iliyopakuliwa kutoka kwa CD, hifadhi au inayopatikana kwenye intaneti,
7. Mwanafunzi atatii sheria zote za hakimiliki.

## Sheria na Masharti ya Tabia Salama ya Basi la Shule

**Matoleo yote ya Kijitabu cha Wanafunzi cha Wilaya ya Shule za Lansing yanatumika kwa wanafunzi ambao ni abiria wa basi la shule.** Isitoshe, lazima kanuni maalum zifuatazo zizingatiwe kwa sababu ya mahitaji ya kipekee ya usalama ya basi linaloenda la shule. Mwanafunzi yeyote anayekiuka kanuni hizi au kutekeleza vitendo vya utovu wa nidhamu kwenye basi anaweza kupewa onyo lililoandikwa la tabia na/au ilani ya kuondoshwa kwa muda. Lazima mwanafunzi aliyeondoshwa kwa muda apokee idhini kutoka kwa mwalimu mkuu kabla ya fadhili za kuabiri basi ziweze kurejeshwa.

1. Dereva wa basi anawajibika kwa basi la shule na usalama wa abiria. **Lazima wanafunzi washirikiane na watii dereva kila wakati.** Ili kuhakikisha usalama wa dereva na abiria, wanafunzi wamekatazwaa kuleta glasi na vitu vingine ambavyo vinaweza kutumika kama silaha (k.m. gongo la besiboli, skuta, ubao mtelezo, n.k.) kwenye basi la shule.
2. Kupanda na kushuka kwenye basi la shule kutadhibitiwa na dereva, mwalimu mkuu na wafanyakazi wa shule.
3. Mlango wa dharura wa kutoka utatumiwa tu kulingana na maagizo ya dereva na haupaswi kuguswa wakati mwingine wowote.
4. Wanafunzi watawasili katika kituo chao cha basi dakika tano (5) kabla ya muda uliopangwa wa kuchukuliwa na watasubiri katika eneo salama kando ya barabara. Wanafunzi wataingia kwenye basi kwa mpangilio na kusalia wameketi na watulivu hadi ifike wakati wa kushuka kwenye gari. Vichwa na mikoni itawekwa ndani ya madirisha ya basi; miguu itawekwa mbali na njia ya katikati na kwenye sakafu wakati wote. Wanafunzi wataagizwa kusimama na kuangalia pande zote kabla ya kuvuka mbele ya basi la shule.
5. Huenda dereva akahitaji wanafunzi kuketi kwenye viti walivyochaguliwa ikihitajika na anaweza kuweka chati ya viti kwa lengo hilo.
6. Maelezo kuhusu vituo vya basi na ratiba itatumwa kwa wanafunzi wote wanaostahiki kabla ya kufungua kwa mwaka wa shule.
7. Hakuna wanyama kipenzi au wanyama wengine watakaoruhusiwa kwenye basi.
8. Wanafunzi walioidhinishwa tu ndio wanaoruhusiwa kwenye basi.
9. Wageni hawawezi kuabiri mabasi ya shule, k.v. wanafunzi watarajiwa, wazazi, wanafunzi wasio wa Wilaya ya Shule za Lansing
10. Njia, vituo, na ratiba za mabasi ya shule zitabainishwana Msimamizi wa Usafiri (Dean Transportation). Mabadiliko yoyote yaliyopendekezwa yatajadiliwa na Afisa wa Uendeshaji wa Wilaya ya Shule za Lansing.

TAFADHALI ZINGATIA
SHERIA NA MASHARTI




YA MAADILI SALAMA
YA BASI LA SHULE

# Taratibu za Tabia Salama ya Basi la Shule

## Maonyo na Kuondoshwa kwa muda

**Kuabiri basi la shule ni fadhila, sio haki.** Ni muhimu kwa wanafunzi kuzingatia maadili salama wakiwa kwenye basi la shule. Dereva wa shule atakuwa na mamlaka ya kutoa onyo lililoandikwa la maadili au pendekezo la kuondoshwa kwa muda kwa mwanafunzi yeyote anayekiuka matoleo ya Kijitabu hiki au anayetekeleza vitendo vingine vya utovu wa nidhamu.

## Utoaji wa Maonyo ya Tabia Mbaya

Dereva atatoa onyo lililoandikwa la maadili, ikiwa kosa ni kali sana kusababisha hatari inayoendelea kwa basi na abiria wake. Katika kisa cha tabia mbaya kupita kiasi, ombi la kuondoshwa kwa muda litawasilishwa kwa mwalimu mkuu.

## Utoaji wa Ilani za Kuondoshwa kwa Muda

Nakala ya onyo la maadili ya basi litatumwa kwa wazazi wa mwanafunzi huyo. Lazima fomu itiwe saini na mzazi na kurejeshwa kwa dereva wa basi na mwanafunzi wakati mwingine anapoabiri basi.

1. Mwalimu mkuu anawajibu wa mwanafunzi kuondoshwa kwa muda kwenye basi.
2. Mwanafunzi ambaye fadhila zake za kuabiri basi zimesitishwa hataweza kuabiri basi kwa kipindi hicho cha kuondoshwa kwa muda. Madereva watapatikana kwa mikutano ya wazazi ikiombwa na mwalimu mkuu. Mwanafunzi aliyeondoshwa asubuhi atasafirishwa nyumbani kwenye basi jioni hiyo.
3. Mwanafunzi ataondoshwa kwenye basi mwisho wa safari ya basi. Katika visa vikali ambapo usalama wa wengine umo hatarini, wanafunzi wa sekondari wanaweza kuondoshwa njiani. Kuondoshwa huko kwa njiani kutaelezewa mwalimu mkuu wa shule mara moja na dereva. Katika tukio la mwanafunzi kuondoshwa kwenye basi shuleni, itakuwa wajibu wa mwalimu mkuu kuwasiliana na wazazi na kupanga jinsi mwanafunzi atafika nyumbani baada ya wanafunzi kondoka darasani. Hakuna wakati wowote mwanafunzi atatumwa nyumbani kwa miguu bila ufahamu na ridhaa ya mzazi. Mwanafunzi aliyeondoshwa kwenye basi kwenda na kutoka shuleni bado ataweza kufikia usafiri uliopangwa mara kwa mara wa wilaya ya shule wa safari za masomo, shughuli za baada ya masomo na hafla nyingine zinazofadhiliwa na shule.

## Malalamiko ya Wanafunzi

Mwanafunzi anayehisi dereva anatekeleza majukumu kwa njia isio salama au isiyofaa anaweza kuwasilisha malalamiko kwa mwalimu mkuu, ambaye atawasiliana na Idara ya Usafiri. Idara ya Usafiri itachunguza malalamiko hayo na kuchukua hatua yoyote inayoonekana inafaa. Matokeo ya uchunguzi yatawasilishwa kwa wazazi aidha kwa maneno au kwa barua punde tu iwezekanavyo.

# Hatua ya Kinidhamu

Kufuata sheria hukuza mazingira salama na yenye mpangilio ambapo masomo yatafanyika. Kila shule itakuwa na mpango wa matokeo bora yanayotokana na kutenda kulingana na kanuni za Shule ambazo zinaweza kujumuisha: utambuzi wa kuongea na wa kuandikwa, fadhila maalum, ripoti za nyumbani, shughuli za kila mwezi na zawadi za maadhimisho.

## Hatua na Athari kwa Wanafunzi katika Kurekebisha Tabia

Wanafunzi ambao hawafuati kanuni za shule watapitia misururu ya hatua zinazohitajika ili kurekebisha tabia hiyo. Shule ya mwanafunzi inawajibika kutoa matokeo ya tabia. Kijitabu hiki kitatumika kwa wanafunzi:

1. Kwenye rasilimali ya shule au katika gari la shule;
2. Waliyomo shuleni au katika shughuli yoyote inayofadhiliwa na shule;
3. Waliyo njiani kwenda na kutoka shuleni au katika shughuli yoyote inayofadhiliwa na shule;
4. Ambao tabia zao mahali au wakati wowote zinaingiliana na shughuli, nidhamu, au maslahi ya jumla ya shule na wanafunzi/wafanyakazi wa shule;
5. Wakati wanatumia mawasiliano yanayomilikiwa na shule au rasilimali za kompyuta na akaunti au huduma nyingine za wilaya.

## Hatua ya Kurekebisha Tabia

Mwanafunzi ambaye anaonyesha tabia ambazo zinatatiza mafunzo na elimu anaweza kuondolewa kwa muda darasani. Katika visa kama hivyo, mwalimu atajaza fomu ya rufaa ya nidhamu na kuiwasilisha kwa mwalimu mkuu kwa wakati kulingana na majukumu ya ualimu, lakini si baada ya mwisho wa siku ya mwalimu isipokuwa hali zisizoepukika zitokee. Ilani ya hatua ya kurekebisha tabia itarekodiwa katika faili ya nidhamu ya mwanafunzi.

## Wazazi Kuarifiwa

Katika kila kisa kinachosababisha kufukuzwa kwa muda, mzazi au mlezi na mwanafunzi (ikiwa ana umri wa miaka 18+), ataarifiwa kwa simu na/au kwa barua siku hiyo ya kufukuzwa. Katika visa vingine vya hatua ya nidhamu, huenda mwanafunzi akaondoshwa shuleni akisubiri uchunguzi wa tukio hilo. Ikiwa hatua

### Matokeo Yaliyoimarika ya Wanafunzi

**Utendaji wa kielimu**
*(Horner et al., 2009)*

**Uwezo wa Kujamii na Kihisia**
*(Bradshaw, Waasdorp, & Leaf, 2012)*

**Matokeo ya Kijamii na Kielimu ya SWD**
*(Lewis, 2017; Tobin, Horner, Vincent, & Swain-Bradway, 2012)*

**Tabia Zinazopungua za Uchokozi**
*(Ross & Horner, 2009; Waasdorp, Bradshaw, & Leaf, 2012)*

**Viwango Vilivyopungua Vilivyoripotiwa vya Wanafunzi Kutumia Dawa za Kulevya au Pombe**
*(Bastable, Kittelman, McIntosh, & Hoselton, 2015; Bradshaw et. al., 2012)*

### Kupunguzwa kwa Adhabu ya Kutengwa

**Rufaa za Adhabu ya Ofisi**
*(Bradshaw, Mitchell, & Leaf, 2010; Bradshaw et al., 2012; Horner et al., 2009)*

**Kuondoshwa**
*(Bradshaw, Mitchell, & Leaf, 2010)*

**Uzuiaji na Kutengwa**
*(Reynolds et al., 2016; Simonsen, Britton, & Young, 2010)*

### Matokeo Yaliyoboreshwa ya Walimu

**Mtazamo wa Ufanisi wa Walimu**
*(Kelm & McIntosh, 2012; Ross, Romer, & Horner, 2012)*

**Hali ya Mpangilio wa Shule na Maisha ya Shule**
*(Bradshaw, Kath, Bevans, Ialongo, & Leaf, 2008; Bradshaw, Kath, Thornton, & Leaf, 2009)*

**Matokeo ya Kijamii na Kielimu ya SWD**
*(Lewis, 2017; Tobin, Horner, Vincent, 7 Swain Bradway, 2012)*

**Mtazamo wa Usalama wa Shule**
*(Horner et al., 2009)*

## Kanuni za Kurejesha Maadili ni nini?

Shughulikia na jadili mahitaji ya jamii ya shule.

Una mahusiano mema kati ya walimu na wanafunzi.

Punguza, zuia, na boresha tabia yenye madhara.

Rekebisha madhara na rejesha mahusiano mema.

Tatua mzozo, hakikisha watu na makundi yanawajibika.

ya nidhamu inahusisha kuondolewa kwa muda, hakuna mwanafunzi ataondolewa kwenye jengo wakati wa saa za shule isipokuwa mzazi, mlezi au mtu mwingine anayewajibika, aliyeorodheshwa kama mtu wa kuwasiliane naye wakati wa dharura, awe amearifiwa. Ikiwa mzazi asiye mlezi, ambaye ameidhinishwa kisheria kufikia rekodi za mwanafunzi, angependa nakala za maelezo ya kuondoshwa kwa muda zitumwe nyumbani mwake, ni wajibu wa mzazi huyo kupatia shule anwani inayofaa.

Ili kuhimiza wanafunzi wetu kukuza tabia salama na inayokubalika, wasimamizi wa shule na wafanyakazi wanaweza kuchukua hatua zinazofaa ambazo zinajumuisha ushauri, urudishaji wa haki, upatanishi, usimamizi wa mizozo na/au rufaa kwa mashirika ya jamii. Wazazi wanapaswa kuwasiliana na mwalimu mkuu wakiwa na wasiwasi wowote.

## Kanuni za Kurejesha Maadili

Haki Adilishi ni mpango wa kutatua mzozo kwa amani ambao unalenga kuwaleta pamoja wanafunzi ambao wamekuwa na mzozo, ili kupata njia za kurekebisha madhara ambayo yamefanyika. Mpango huu unalenga hali za mzozo shuleni kwa kuwahusisha wahusika wote walioathiriwa.

Wawezeshaji Haki Adilishi wamo shuleni na wanapatikana hali zikiibuka shuleni. Haki Adilishi hushughulikia mgongano kuanzia kwa shina, huku ukikuza ujuzi wa kutatua mzozo na huruma.

Mchakato wa Haki Adilishi ni kama ufuatao:

1. **Rufaa:** mwanafunzi huelekezwa kwa Haki Adilishi na wafanyakazi, wasimamizi, au kivyako
2. **Kukubaliwa:** wawezeshaji hukutana na wahusika wote ili kuzungumzia kuhusu kilichofanyika, madhara yaliyofanyika, na yale wanafunzi wanahitaji ili kuendelea mbele. Baada ya kuzungumza na mwanafunzi kivyake, mwanafunzi huamua kama angetaka kushiriki katika mkutano wa kungilia kati
3. **Mkutano:** Wahusika wote huletwa pamoja kwa mkutano, ambapo wasimamizi huongoza mazungumzo. Wanafunzi huulizwa ni nini kilichofanyika kulingana na mtazamo wao, ni nani aliyeathiriwa na aje, na ni nini kinachopaswa kufanyika ili kurekebisha madhara
4. **Makubaliano:** Kisha wanafunzi huunda makubaliano kuhusu jinsi wanavyopanga kuendelea mbele kutoka kwa hali hiyo, wakisema jinsi watatua mzozo huo, jinsi wanaweza kuepuka mzozo huo baadaye, na jinsi wanavyopanga kushughulikia hali hizo baadaye
5. **Ufuatiliaji:** Wawezeshaji uhitimisha mkutano huo kwa Utafiti Mfupi, unaowauliza wanafunzi jinsi wanavyohisi mchakato huo ulienda. Siku ishirini na moja baada ya mkutano wa kuingilia kati, wawezeshaji watafuatilia kwa Utafiti Mrefu, wa kuona jinsi wanafunzi wanavyoendelea baada ya mzozo wao

### Matokeo Yanayonuiwa

Haki Adilishi hushughulikia mzozo kuanzia kwa shina yake:

1. Kushurutisha uwajibikaji na kuwawezesha wale ambao wamekosa kurekebisha madhara yaliyosababishwa na tabia zao;
2. Kuwawezesha wale ambao wameumizwa kufafanua wanayohitaji ili kupata nafuu kutokana na madhara yaliyofanywa; Huwafunza na kuwahusisha vijana (na wakati mwingine familia zao) katika kanuni za kutatua mizozo kwa amani."

Haki Adilishi ni njia jumlishi za kutia nidhamu bila kuadhibiwa.

Haki Adilishi ni hatua zinazowalenga wanafunzi ambazo zimebuniwa kuanzisha mahusiano mema na wanafunzi wote (Kline, 2016). Kuna sehemu amilifu na ya jibu za haki adilishi ambazo zinaweza, na pengine zinapaswa, kufanya kazi kwa pamoja ili kuleta matokeo yanayohitajika zaidi (Watchel, 2013). Sehemu "amilifu" ya haki adilishi hulenga kuunda mazingira ya haki na sawa ya masomo na kukuza mahusiano mema; huku sehemu "ya jibu" ikilenga kurekebisha madhara na kubadlisha mizozo (Evans & Vaandering, 2016).

## Ukaguzi na Upokonyaji

**Ukaguzi:** Ukaguzi wa wanafunzi, mali ya kibinafsi ya wanafunzi, na magari utatekelezwa kulingana na kiwango kinachofaa cha sheria, ili kudumisha usalama wa wanafunzi, walimu, wageni na mali ya shule.

**Wafanyakazi Waliodhinishwa:** Wafanyakazi waliodhinishwa kutekeleza ukaguzi watakuwa mwalimu yeyote mkuu, mwalimu mkuu msaidizi, wanachama wa Idara ya Usalama wa Umma, au afisa yeyote mwingine wa shule aliyeteuliwa na mwalimu mkuu kutekeleza ukaguzi.

### Ukaguzi wa Wanafunzi

Wafanyakazi waliodhinishwa wanaweza kutekeleza ukaguzi kwa mwanafunzi, mfuko wa vitabu, begi, au mali yoyote ile ya mwanafunzi ikiwa wana shaka ya kutosha ya kutekeleza ukaguzi huo. Katika hali maalum, ukaguzi usiokuwa na utaratibu maalum unaweza kuhitajika. Shaka ya kutosha ya kutekeleza ukaguzi hurejelea hali ambazo zinaweza kusababisha mtu kuamini kwamba ukaguzi wa mtu, mahali au kitu fulani utasababisha utambuaji wa:

1. Ushahidi wa ukiukaji wa sheria yoyote ya ndani au ya jimbo/serikali;

2. Ushahidi wa ukiukaji wa Kijitabu hiki au sera yoyote nyingine ya Bodi ya Elimu au sheria za usimamizi;





3. Kifaa chochote ambacho kinaweza kusababisha hatari au madhara ya kimwili au ugonjwa kwa mwanafunzi, mfanyakazi, mgeni, yeyote au mali ya shule, iwe kwenye rasilimali ya shule, tukio linalofadhiliwa na shule au kwenda na kurudi kutoka shuleni.

Baada ya shaka ya kutosha na ili kulinda afya, usalama, au maslahi ya wanafunzi wanaosimamiwa na wilaya ya shule, mwalimu mkuu au mwakilishi wake anaweza kuwakagua wanafunzi. Watu wazima wawili watakuwepo wakati wa ukaguzi wa mwanafunzi.

Ikiwa mwanafunzi atakataa kutii, jaribio litafanywa la kuwasiliana na mzazi na suala hilo litaelekezwa kwa Idara ya Usalama wa Umma au shirika lingine lolote la kutekeleza sheria, kama inavyofaa. Idara ya Usalama wa Umma au shirika lingine la utekelezaji wa sheria litatekeleza ukaguzi wa kimwili wa mwanafunzi kama inavyoruhusiwa chini ya sheria.

## Ukaguzi wa Makabati

Makabati yote katika Wilaya ya Shule za Lansing ni mali ya wilaya na yako chini ya usimamizi wa mwalimu mkuu wa shule au mwakilishi wake. Hakuna wakati wowote wilaya itaondoa udhibiti wake wa pekee wa makabati yake. Wanafunzi wamekatazwa kuweka vifuli vya kibinafsi kwenye makabati ya shule. Wafanyakazi walioidhinishwa wataondoa vifuli vyovyote binafsi kwenye makabati ya shule.

Makabati ya shule hupewa wanafunzi ili kuwasaidia na kutumiwa kwa muda. Wanafunzi wanapaswa kutumia makabati ya shule kuhifadhi nyenzo zinazohusiana na shule pekee na vitu vya kibinafsi vilivyoidhinishwa na shule kama vile mavazi, viatu, mapambo na chakula cha mchana. Wanafunzi wanawajibika kwa yaliyomo kwenye makabati yao na hawawezi kushiriki makabati yao au nambari ya kabati na wanafunzi wengine.

Ukaguzi usiokuwa na mpangilio maalum wa makabati ya shule utatekelezwa. Wafanyakazi waliodhinishwa wanaweza kukagua makabati na yaliyomo kwenye makabati wakati wowote ule, bila ilani na bila ridhaa ya mwanafunzi au mzazi/mlezi. Mbwa aliyeidhiniwa wa kugundua na mkufunzi wake wanaweza kutumiwa kutekeleza ukaguzi usiokuwa na mpangilio maalum kwenye makabati. Watu wawili (2) wazima watakuwepo wakati wa ukaguzi wa makabati.

Ikiwa afisa wa kutekeleza sheria anayetaka kukagua kabati la mwanafunzi ana kibali cha ukaguzi, mwalimu mkuu au mwakilishi wake atampeleka afisa huyo mara moja kwa kabati la mwanafunzi na kumruhusu kulikagua. Ikiwezekana, ukaguzi kama huo utafanyika katika uwepo wa mwalimu mkuu au mwakilishi wake. Afisa wa kutekeleza sheria anaweza kukagua kabati bila kibali cha ukaguzi ikiwa atapewa ridhaa ya kukagua na mtu ambaye ni mwenye kabati hilo.

Ikiwa afisa wa kutekeleza sheria, kando na afisa wa Idara ya Usalama wa Umma wa Wilaya ya Shule za Lansing, anataka kukagua kabati lililopewa mwanafunzi bila kibali, mwalimu mkuu au mwakilishi wake atauliza sababu zinazosababisha afisa huyo kuamini kwamba ushahidi wa uhalifu utapotea, kuharibiwa au kuhamishwa ikiwa ukaguzi au upokonyaji haukufanyika mara moja, kabla ya kibali kupatikana. Ikiwa mwalimu mkuu wa shule au mwakilishi wake hakubaliani na afisa, atamruhusu afisa kuendelea kwa mamlaka yake mwenyewe lakini hatashiriki katika ukaguzi huo. Mwalimu mkuu au mwakilishi wake ataripoti mara moja tukio hilo kwa Mkurugenzi wa Usalama wa Umma, ambaye ataarifu mkuu wa afisa huyo kuhusu tukio hilo.




## Upokonyaji

Vitu vinavyoaminika kuhusishwa na shughuli zisizo halali au zinazokiuka Kijitabu hiki, sera ya Bodi, kanuni za usimamizi, au vinavyosababisha hatari ya madhara ya kimwili au ugonjwa kwa mwanafunzi, mfanyakazi, mgeni yeyote au mali ya shule vinaweza kupokonywa na mtu anayetekeleza utafiti. Vitu vyovyote vilivyopokonywa kama matokeo ya ukaguzi vitakabidhiwa Idara ya Usalama wa Umma au shirika la kutekeleza sheria. Vitu vilivyochukuliwa vinaweza kosa kurejeshwa.

## Ukaguzi wa Magari

Wafanyakazi waliodhinishwa wanaweza kukagua gari lolote lililoingia kwenye rasilimali ya shule na mwanafunzi wakati wowote baada ya shaka ya kutosha kwamba gari hilo lina:

1. Ushahidi wa ukiukaji wa sheria yoyote ya ndani au ya jimbo/serikali;
2. Ushahidi wa ukiukaji wa Kanuni au sera yoyote nyingine ya Bodi ya Elimu au sheria za usimamizi;
3. Kifaa chochote ambacho kinaweza kusababisha hatari au madhara ya kimwili au ugonjwa kwa mwanafunzi, mfanyakazi, mgeni, yeyote au mali ya shule, iwe kwenye rasilimali ya shule, tukio linalofadhiliwa na shule au kwenda na kurudi kutoka shuleni.

Ukaguzi kama huo unaweza kutekelezwa bila ilani kwa mwanafunzi. Wanafunzi wanaokataa kushirikiana katika kuruhusu ukaguzi wa gari watapoteza fadhila zao za kuendesha gari na kuegesha na wanaweza kuchukulia hatua zaidi za kinidhamu kama ilivyoelezwa katika Kijitabu hiki.

Ili kulinda afya, usalama au masilahi ya wanafunzi na jamii ya shule, watekelezaji sheria watahusishwa ili kusaidia katika kukagua gari hilo lililoletwa kwenye rasilimali ya shule na mtu asiyekuwa mwanafunzi. Mbwa aliyeidhiniwa wa kugundua na mkufunzi wake wanaweza kutumiwa kukuza shaka ya kutosha na kuanzisha ukaguzi.

## Matumizi ya Dharura ya Utengaji au Uzuiaji

Huenda utengwaji wa dharura usitumike zaidi ya inavyohitajika kwa mwanafunzi kupata udhibiti.

- Usizidishe dakika 15 kwa shule ya msingi;
- Usizidishe dakika 20 kwa shule ya kati/ya upili;
- Ikiwa ni zaidi ya dakika 15/20:
    - Huenda msaada wa ziada ukahitajika (k.m. mfanyakazi, muuguzi mbadala, au mfanyakazi muhimu wa ziada.)



## Kuingilia kati Kibinafsi au Kutengwa na Wafanyakazi

Wilaya za shule za karibu zinaruhusiwa kubuni, kutumia na kutekeleza sera yao sambamba na sera ya jimbo au kutumia sera ya jimbo kwa matumizi ya dharura ya kuzuiwa na kutengwa. Hata hivyo, Lansing School District inafuata mwongozo wa jumla wa masuala ya Kutengwa kwa Dharura na Kuzuiwa Kihalisi kutoka Idara ya Elimu ya Michigan (MDE) kama ilivyoidhinishwa na Bodi ya Elimu ya Jimbo tarehe 14 Machi 2017 na kusasishwa Julai 2017.

Wilaya ya Shule za Lansing haziwaruhusu wafanyakazi kutumia adhabu ya viboko (matumizi au vitisho vya adhabu ya kimwiili ili kubadilisha tabia) kwa mwanafunzi. Uzuiaji wa Kimwili wa Dharura unahusisha mgusano wa moja kwa moja wa kimwili au kuzuia pakubwa mwenendo wa mwanafunzi. Uzuiaji wa Kimwili wa Dharura ndio hatua ya mwisho ya usalama ya dharura

Wafanyakazi wanaruhusiwa kutumia kizuizi cha kimwili (badala ya 'nguvu') kwa mwanafunzi ili:

1. Kujilinda wenyewe au mtu mwingine dhidi ya mashambulizi ya kimwili
2. Kumzuia mwanafunzi kujiumiza mwenyewe
3. Kukomesha usumbufu ambao unaweza kusababisha majeraha ya kimwili kwa mtu yeyote
4. Kupata umiliki wa silaha au vitu vingine hatari
5. Kulinda mali: Iwapo kitendo cha kuharibu mali kinasababisha hatari kwa usalama wa mwanafunzi au mfanyakazi, hatua ya dharura ya kutumia sera ya kutengwa na kuzuiwa kihalisi inaruhusiwa
6. Mzindikishe kimwili mwanafunzi ambaye anashiriki katia tabia inayotatiza mazingira ya elimu na ambaye ameshindwa kutii maagizo ya maneno ya kukomesha tabia kama hiyo. Kuzindikishwa kimwili ni kumgusa au kumshilikia mwanafunzi kwa kupunguza mgusano kwa lengo la kuelekeza mwenendo kutoka mahali pamoja hadi pengine
7. Wilaya ya shule ina haki ya kuongea na wanafunzi ili kuchunguza tatizo au matatizo yanayotokea shuleni, kwenye basi, na katika shughuli zinazohusiana na shule.

Hatua hiyo itakuwa salama, inayofaa, mwafaka na nyeti kwa hali ya tabia, umri, awamu ya kukua, ukubwa wa kimwili, jinsia, hali za kimatibabu za kimwili na kisaikolojia, na historia ya kibinafsi (unyanyasaji wa kimwili au kingono au kiwewe).

Zifuatazo ni mifano ya makosa ambayo wanafunzi wanaweza kuadhibiwa. Hatua mahsusi ya nidhamu itabainishwa kulingana na ukali wa kosa na hali husika.

### Kiwango cha 1 – Makosa Madogo

Tabia ambazo zina athari mbaya kwa mazingira ya shule.

### Kiwango cha 2 – Makosa ya Wastani/ya Kurudiwa

Tabia ambayo inatatiza na kuingilia pakubwa mazingira ya shule, lakini si hatari kwa wanafunzi, watu wengine, au mali, AU haisababishi majeraha makubwa.

### Kiwango cha 3 – Makosa Makubwa

Tabia ambayo ni hatari kwa afya na usalama wa wanafunzi, marafiki, wafanyakazi, au mali. Utovu wa nidhamu unaokithiri ambao hausuluhishwi kwa mbinu nyingine.

**Lugha ya Matusi (kiwango cha 1- 4)** Ujumbe wa kutamka ambao unatumia maneno kwa njia isiyofaa na unaweza kujumuisha, lakini si tu kwa kuitana majina, na matusi.

**Pombe (kiwango cha 2- 6)** Umiliki na matumizi ya pombe na/au bidhaa zisizo za pombe ni marufuku. Pombe, ambayo inajulikana kwa jina lake la kemikali ethanoli, ni dawa inayobadilisha utendakazi wa mfumo wa neva ambayo ndio kiungo kinachotumika katika vinywaji kama vile bia, mvinyo, na vinywaji vikali (pombe kali). Inazingatiwa kuwa bidhaa ya burudani, inayosababisha mabadiliko ya kitabia ya kulewa ("ulevi").

**Uchomaji (kiwango cha 6)** Kuchoma kwa makusudi au jaribio la kuchoma jengo au mali au jengo lolote ya, inayokodishwa na, au kwenye mkopo wa wilaya ya shule au mali ya mtu yeyote.

**Ushambulizi (Wa kimwili) (kiwango cha 3-6)** kusababisha au kujaribu kusababisha madhara ya kimwili kwa makusudi kwa mtu mwingine kwa nguvu au ukatili (k.m. wafanyakazi au wanafunzi).

**Tishio la Bomu (kiwango cha 3-6)** Kutoa tishio la bomu au tishio lingine kama hilo katika jengo la shule, mali nyingine ya shule, au tukio linalohusiana na shule.

**Maonevu (kiwango cha 1- 6)** yanafafanuliwa kama kitendo chochote kilichorudiwa ambacho kimeandikwa, kutamkwa, au kimwili, ikiwemo maonevu ya mtandaoni [k.v. mawasiliano yoyote ya elektroniki, ikiwemo, lakini hayajakomea kwa vitendo vinavyotekelezwa kupitia elektroniki, kama vile intaneti, simu, au simu ya mkononi, kisaidizi binafsi cha dijitali (PDA), au kifaa pasiwaya cha mkononi] ambacho, bila kujali mhusika au sababu, kimekusudiwa au kwamba mtu mwenye busara anaweza kujua kinaweza kusababisha madhara kwa mwanafunzi mmoja (1) au zaidi aidha moja kwa moja au kwa njia isio ya moja kwa moja kwa kufanya chochote kati ya zifuatazo:

1. Kutatiza pakubwa nafasi, faida, au mipango ya elimu ya mwanafunzi mmoja (1) au zaidi;
2. Kuathiri pakubwa uwezo wa mwanafunzi wa kushiriki au kufaidika na mipango au shughuli za kielimu za wilaya ya shule kwa kumfanya mwanafunzi awe na hofu ya kuumizwa kimwili au kusababisha dhiki kubwa ya kihisia;
3. Kusababisha athari halisi na kubwa kwa afya ya kimwili au kiakili ya mwanafunzi; na/au
4. Kusababisha usumbufu mkubwa, au kuingilia sana shughuli za kawaida za shule.

Maonevu yanaweza kuwa ya kimwili, ya maneno, kisaikolojia, au mchanganyiko wa zote tatu. Baadhi ya mifano ya maonevu ni:

1. Ya kimwili: kugonga, kurusha teke, kutema mate, kusukuma, kuvuta, kuchukua na/au kuharibu mali ya mtu, kupokonya pesa, kuzuia mwenendo wa mwanafunzi, kumgusa mtu bila hiari yake.

2. Ya maneno: kudhihaki, kukejali kwa nia mbaya, kutusi, kuitana majina, kutoa vitisho.

3. Ya kisaikolojia: kueneza uvumi, kuharibu mahusiano ya kijamii, kulazimisha, au kushiriki katika kutengwa/kuepukwa, kupokonywa, au kutishwa. Hii inaweza kufanyika kwa njia mbali tofauti, ikiwemo lakini si tu kwa vidokezo, barua pepe, machapisho ya mitandao ya kijamii, na michoro.

4. Maonevu ya mtandaoni: mawasiliano yoyote ya elektroniki, ikiwemo, lakini si tu vitendo vinavyotekelezwa kupitia elektroniki, kama vile intaneti, simu au simu ya mkononi, kisaidizi binafsi cha dijitali (PDA), au kifaa pasiwaya cha mkononi.

5. Unyanyasaji au vitisho vya Kijamii/Kimbari: Kitendo cha nia mbaya na cha makusudi cha kunyanyasaji au kumtisha mtu mwingine kwa sababu ya rangi, asili ya kijamii au mbari ya mtu huyo.

6. Unyanyasaji wa Kingono au Vitisho*: Utongojozaji wa kingono usiotakikana, kejeli, vichekesho, maoni, au maswali, aidha ya maneno au ya kimwili, kuwadia mtu mwingine kwa sababu ya jinsia yake au mwelekeo wa kingono. Unajumuisha pia maombi ya fadhila za kingono au tabia nyingine za maneno au kimwili za kingono ambapo tabia hiyo ina lengo au athari ya kutatiza utendakazi wa kielimu wa mwanafunzi kwa kuunda mazingira ya kutisha, mabaya au ya kukera ya kielimu.

Wilaya ya Shule za Lansing imepiga marufuku unyanyasaji wa kingono kinyume na sheria. Marufuku haya yanasimamia mwenendo usiofaa wa kingono kuwadia wanafunzi na wanafunzi, wafanyakazi wa Wilaya, Wanabodi au wachuuzi wa shule, shule au katika tukio au shughuli inayofadhiliwa na shule.

Mwanafunzi yeyote anayeamini kuwa amepitia unyanyasaji wa kingono uliopigwa marufuku anapaswa kuripoti mara moja kwa mwalimu mkuu, mwalimu au mmoja wa **Maafisa wa Utekelezaji wa Wilaya (angalia ukurasa wa 5)**. Wazazi wanaweza pia kuripoti hoja hizi.

Wanafunzi na wafanyakazi wanaopatikana wakihusika katika vitendo vya mwenendo usiofaa wa kingono-ambavyo vinaweza kujumuisha vitendo visivyotakikana au vya kulazimishwa vya kingono au tabia ya hali ya kingono- wataadhibiwa mara moja. Adhabu inaweza kujumuisha, Ikiwa hali inaruhusu, kuondoshwa kwa muda au kufukuzwa kwa mwanafunzi, au mfanyakazi kusimamishwa kazi.

**Udanganyifu/Wizi wa maandishi (kiwango cha 1-4)** Kuwasilisha kazi ya uongo kama kazi yako mwenyewe ya asili au kuwapa wengine majibu ya mitihani au kazi ya kunakili. Ubora wa kazi hautazingatiwa katika kubainisha hatua ya kinidhamu.

**Tabia isiyo ya kawaida (kiwango cha 1- 6)** Tabia yoyote ndani au nje ya shule, ikiwemo darasani, ambayo ni hatari au inatatiza na kutishia usalama wa wanafunzi, au wengine, ikiwa ni pamoja na mtu aliye na mwenendo usiofaa. Hii inajumuisha lakini haijakomea kwa: kutupa mipira ya theluji, mawe, au vitu vingine; kuzuia kamera za usalama; kusukuma; kupiga kelele; au kukimbia ukumbini; na kuchochea, kutazama au kuongezea makosa ambayo wanafunzi wataadhibiwa. Kuwa mtazamaji katika hali ya maonevu au vita inaweza kuchukuliwa kama mwenendo usiofaa.

**Matumizi Mabaya ya Vifaa vya Mawasiliano ya Elektroniki (ECD) (kiwango 1-3)** Kifaa cha elektroniki ambacho kina uwezo wa kupitisha ujumbe kupitia matumizi ya intaneti, vifurushi vya data, au maeneo mengine ya kufikia Wi-Fi. Umiliki wa ECD unaruhusiwa kulingana na maagizo yaliyoorodheshwa kwenye ukurasa wa 18 na 19 wa Mwongozo huu.

**Unyanyasaji au vitisho vya Kijamii/Kimbari (kiwango cha 1-5)** Kitendo cha nia mbaya na cha makusudi cha unyanyasaji au kumtisha mtu mwingine kwa sababu ya rangi, asili ya kijamii au mbari ya mtu huyo.

**Vilipuzi/Vifaa vya Kuteketeza (kiwango cha 1-6)** Uuzaji, umiliki, au matumizi ya vilipuzi au vifaa vya kuteketeza ikiwemo mabomu na fataki.

**Uporaji/Wizi (kiwango cha 2-6)** Kupata pesa au mali (kitu chenye thamani) kutoka kwa mtu asiyetaka aidha kwa nguvu au vitisho.

**Maonyo Bandia/Simu za 911 (kiwango cha 2-5)** Kuwasha mfumo wa kingora cha moto bila sababu na/au kupigia simu Kituo cha Dharura cha 911 kwa nia mbaya katika jengo lolote la shule au mali ya shule.



* Wilaya ya Shule ya Lansing inachukua madai ya uwongo kwa uzito. Rejea kwa ukurasa wa 30 kwa matokeo ya madai ya uwongo ya hujumu ya kingono au unyanyasaji.

**Madai ya Uongo ya Mashambulizi au Unyanyasaji wa Kingono** Wanafunzi kutoa ripoti ya uongo kwa makusudi, kuwasilisha Malalamiko Rasmi ya uongo, kutoa taarifa ya uongo au kuwasilisha maelezo ya uongo wakati wa mchakato wa malalamiko wa Tittle IX unazingatiwa kuwa kosa la kukiuka Kijitabu cha Wanafunzi. Kwa makosa kama hayo, wanafunzi wanaweza kuwajibika kulingana na Matriksi ya Nidhamu/Kuingilia kati.

**Kupigana (kiwango cha 2-6)** Mgusano wa kimwili ambapo mangumi yanarushiwa mtu mwingine. Tafadhali kumbuka matokeo ya mwanafunzi kupigana katika gredi ya K-6 ni kama yafuatayo: Kosa la kwanza 1 kuondoshwa shuleni siku moja (1) hadi tisa (9); kosa la 2 linaweza kusababisha kupelekwa kwenye Ofisi ya Utamaduni wa Shule na nyaraka ya Vipengele 7, vita vinavyofuata - kupelekwa kwenye Ofisi ya Utamaduni wa shule na uwezekano wa kufukuzwa.

Tafadhali kumbuka matokeo ya mwanafunzi kupigana katika gredi ya 7-12 ni kama yafuatayo: Kupigana mara ya **1 na ya 2** ; Kuondolewa kwa siku 3-9; **Kupigana zaidi ya mara 2** Kuripotiwa kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule kunaweza kusababisha kuondolewa shuleni kabisa.

**Kughushi (kiwango cha 1-5)** Kutumia au kuandika jina au utambulisho wa mtu mwingine kwa malengo ya kupata, au kubadilisha saa, tarehe, gredi, anwani, au maelezo mengine, ikiwemo fomu za shule.

**Kucheza kamari (kiwango cha 1-5)** Kucheza kamari ni kinyume cha sheria na kunaweza kusababisha kuondoshwa shuleni. Kucheza kamari ni kukubali pesa au kitu chochote chenye thamani kwa kutegemea tukio lisilojulikana.

**Shughuli za Magenge (kiwango cha 1-6)** Kuonyesha zana za magenge au kuonyesha tabia au ishara ambazo zinaashiria uanachama wa magenge; kuanzisha, kutetea, au kukuza shughuli ambazo zinatishia usalama wa maslahi ya wengine au kushiriki katika shughuli zinazolenga kuwatishia wengine; kushiriki katika tabia zinazolenga shughuli za kuingizwa katika genge.

**Udhalilishaji (kiwango cha 1-5)** Kuwafanya wengine wapitie kejeli au matusi ambayo yanaleta hatari ya majeraha ya kimwili, kiakili au kihisia ambayo ni lazima mtu avumilie ili awe mshiriki wa darasa, shirika au kundi. Mtu kuwa tayari kuingizwa katika kundi hakutazingatiwa katika kubainisha hatua ya nidhamu.

**Kutotii (kiwango cha 1- 5)** Kushindwa kutii, kufuata, au kutekeleza maagizo kutoka kwa mfanyakazi yeyote wa shule (mwalimu mkuu, mwalimu, mlezi, mfanyakazi wa kafeteria, wafanyakazi wa usalama, msaidizi au dereva wa basi).

**Kuhofisha/Unyemeleaji/Vitisho (kiwango cha 1-6)** Kumweka mtu mwingine katika hofu ya kuumizwa kimwili kwa kutumia maneno au tabia nyingine za kutishia, lakini bila kuonyesha silaha au kumfanya mtu kushambuliwa kimwili. Unajumuisha pia tabia yoyote (iliyoandikwa, kutumkwa au ya kimwili) ambayo ina lengo au athari ya kutatiza utendakazi au kielimu wa mwanafunzi kwa kuunda mazingira ya kutisha, mabaya, au ya kukera ya kielimu.

**Uharibifu wa nia mbaya (kiwango cha 1-6)** Uharibifu wa makusudi au kuchafua mali, inayokodiwa, au kwenye mkopo wa mfumo au mali ya shule (pamoja na magari) ya watu walioajiriwa na shule au wanaoenda shule.

**Bangi na vitu vingine vinavyodhibitiwa (kiwango cha 2-6)** Mauzo, Matumizi, Umiliki, au Usambazaji wa dawa halali au zisizo halali, na au zana za dawa za kulevya zimepigwa marufuku. Sera hii inajumuisha, lakini haijakomea kwa, vyakula/vinywaji vyenye vitu vilivyothibitishwa (dawa zinazoweza kuliwa au zinazofanana na nyingine). (Hazijumuisha dawa zilizotumiwa kulingana na Sheria ya Usimamizi Nambari 5141.3). Matokeo ya kumiliki/kutumia dawa halali au zisizo halali na/au zana zake ni kama yafuatayo: **kosa la 1** kuondoshwa shuleni kwa siku 3-9 na kuelekezwa kwa shirika la nje kwa kutumia dawa za kulevya; **kosa la 2** linaweza kusababishwa kupelekewa kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule na mazingatio ya nyaraka za Vipengele 7 na kuelekezwa kwa shirika la nje kwa kutumia dawa za kulevya.

**Tabia Chafu au Iliyopotoka (Kiwango cha 1-5)** Kitendo cha kutumia lugha chafu au najisi kwa njia ya kuzungumza au kuandika, kumiliki picha za ponografia, kufanya ishara au vitendo vya kukera au kushiriki katika tabia ya hali ya kingono kwenye mali ya shule, basi la shule au katika tukio au shughuli inayofadhiliwa na shule.

**Kumiliki au Kutumia Bunduki ya Kuchezea/Fanani au Mfano wa Silaha (kiwango cha 1-6)** Kumiliki au kutumia silaha fanani/bunduki ya kuchezea, au mfano wa silaha. Mifano inajumuisha: bunduki za kuchezea,

au vitu vya jukwaani, bastola za kuanzisha mbio, sanamu, vifanani au kifaa kingine chochote kilichoundwa au kutumiwa kuiga silaha. Silaha hizi fanani/bunduki za kuchezea HAZIWEZI kurusha risasi.

**Umiliki au Matumizi ya Bunduki za Airsoft (kiwango cha 1-6)** Umiliki au matumizi ya Bunduki ya Airsoft au silaha yoyote ambayo inarusha vitu visivyoweza kuumiza kama vile peleti za plastiki ambazo zinawezeshwa na gesi, hewa iliyofinyazwa, au kurushwa kwa springi. Bunduki za Airsoft/bunduki za BB zinazingatiwa kuwa silaha na HAZIWEZI kujumuishwa katika ufafanuzi huu.

**Mashambulizi ya Kingono (kiwango cha 1-6)*** Wilaya ya Shule za Lansing itachunguza mara moja ripoti na kubainisha kadri ambayo kumekuwa na ukiukaji wowote wa Kijitabu cha Wanafunzi cha wilaya. Wilaya ya Shule za Lansing imepiga marufuku vitendo vya kingono kati ya wanafunzi shuleni, kwenye basi la shule, au katika shughuli au tukio linalodhaminiwa na shule. Wilaya haitavumilia vitendo dhidi ya wanafunzi ambavyo ni vya mashambulizi ya kingono au mwenendo wowote wa kingono.

Mashambulizi ya Kingono yanafafanuliwa kisheria/kijinai kama Mwenendo wa Kingono wa Jinai katika ngazi ya kwanza hadi ya nne, ambayo inajumuisha kitendo chochote cha kingono dhidi ya mtu mwingine, kwa lazima na/au kinyume na ari ya mtu, au kitendo chochote kisicho cha lazima cha kingono kinyume na ari ya mtu ambapo mhadhiriwa hawezi kutoa ridhaa na ambapo nguvu au kulazimishwa kunatumiwa au kutishiwa. Matumizi ya utawala ni aina ya kulazimishwa.

Mtu mwenye umri wa miaka 15 au chini hawezi kisheria kutoa ridhaa ya vitendo vya kingono. Lansing School District imepiga marufuku vitendo vya ngono bila kujali umri. Ikiwa kitendo kama hicho kitafanyika shuleni, kwenye basi la shule, au katika tukio au shughuli inayodhaminiwa na shule, mwanafunzi anapaswa kuripoti kitendo hicho kwa wafanyakazi wa Wilaya ya Shule za Lansing (k.v. mwalimu mkuu, mwalimu, usalama wa umma, au Maafisa wa Utekelezaji wa wilaya) na maafisa wa kutekeleza sheria. **Uchunguzi wa Title IX utafanywa na mratibu wa wilaya wa Title IX na usalama wa umma utaripoti vitendo vyote vinavyohusiana na ngono kwa watekelezaji wa sheria ili vikaguliwe zaidi.**

Sera ya Title IX/hatua za mpito zinaweza kutumika katika matukio ambayo yalifanyika nje ya shule, na/au kabla na baada ya shule.

Shughuli au tabia yoyote ya kingono kati ya wafanyakazi wa Wilaya na wanafunzi ni ukiukaji wa sera ya Bodi, imepigwa marufuku na lazima iripotiwe kwa wafanyakazi wa Wilaya, ikijulikana. Wanafunzi wanahimizwa kuripoti mara moja tabia zote kama hizo kwa **Maafisa wa Utekelezaji wa Wilaya (angalia ukurasa wa 5)**, mwalimu wako mkuu au mtu mwingine mzima anayeaminika.

**Unyanyasaji wa Kingono (kiwango cha 1 - 6*)** Utongozaji wa kingono usiotakikana, kejeli, vichekesho, maoni, au maswali, aidha ya maneno, yaliyoandikwa, au matumizi ya ishara za dhahiri za kingono kuwadia mtu mwingine kwa sababu ya jinsia yake au mwelekeo wa kingono. Hii pia inajumuisha maombi ya fadhila za kingono au tabia nyingine za maneno au kimwili za kingono ambapo tabia hiyo ina lengo au athari ya kutatiza utendakazi wa kielimu wa mwanafunzi kwa kuunda mazingira ya kutisha, mabaya au ya kukera ya kielimu. (Vitisho vya kingono vimejumuishwa chini ya "Kuhofisha/Unyemeleaji/Vitisho")

Mwenendo unachukuliwa kuwa hautakikani ikiwa mwanafunzi hakuuomba au kuutaka na huzingatia kuwa usiotakikana au unaokera. Umri wa mwanafunzi, hali ya mwenendo, na mambo mengine muhimu yanaathiri kama mwanafunzi aliweza kukubali mwenendo wa kingono.

Mwanafunzi kukubali mwenendo huo au kushindwa kulalamika hakumaanishi kila wakati kwamba mwenendo huo unakubalika.

***Mfano wa 1:*** Mwanafunzi anatoa vichekesho vya kingono vya kukera kwa mwanafunzi mwingine, lakini mwanafunzi huyo hapingi vichekesho hivyo au kuvizungumzia. Kushindwa kwa mwanafunzi kupinga hakumanaishi kwamba amekubali maoni hayo.

***Mfano wa 2:*** Mwanafunzi #1 kwa makusudi anamtumia busu mwanafunzi #2 katika tukio moja shuleni. Siku inayofuata ya shule, akiwa kwenye basi la shule, mwanafunzi #1 anamtumia busu, tena, mwanafunzi #2 na anatumia ishara dhahiri za kingono kuwadia mwanafunzi wa 1. Mwanafunzi #1 anatabasamu, lakini hajibu au kuripoti. Kwa sababu mwanafunzi #1 hakujibu au kuripoti, haimaanishi amekubali tabia hiyo.

Wilaya ya Shule za Lansing imepiga marufuku vitendo vya kingono kati ya wanafunzi shuleni, kwenye basi la shule, au katika shughuli au tukio linalodhaminiwa na shule. Wilaya haitavumilia vitendo dhidi ya wanafunzi ambavyo ni vya mashambulizi ya kingono au mwenendo wowote wa kingono.



* Wilaya ya Shule ya Lansing inachukua madai ya uwongo kwa uzito. Rejea kwa ukurasa wa 30 kwa matokeo ya madai ya uwongo ya hujumu ya kingono au unyanyasaji.

Sera ya Title IX/hatua za mpito zinaweza kutumika katika matukio ambayo yalifanyika nje ya shule, na/au kabla na baada ya shule.

**Ujumbe mchafu na Ponografia ya Watoto (kiwango cha 1- 6)** Kitendo cha kushiriki au kuonyesha picha za uchi au picha zako na/au za wanafunzi wengine, kupitia mitandao ya kijamii au vinginevyo. Mtu yeyote kwa makusudi anapotengeneza, kusambaza, au kumiliki ponografia ya watoto atakuwa amekiuka Kifungu cha Sheria cha Michigan (750.145c). Nyenzo za ponografia ya watoto ni onyesho lolote, picha, filamu, slaidi, video, picha ya kuonekana ya elektroniki, kompyuta au picha inayozalishwa na kompyuta au rekodi ya sauti ambayo ni ya mtoto (chini ya umri wa miaka 18) au inayoonekana kujumuisha mtoto akihusika katika kitendo cha ngono. Huenda picha ikajumuisha filamu au negativu isiyotengenezwa.

Sera ya Title IX/hatua za mpito zinaweza kutumika katika matukio ambayo yalifanyika nje ya shule, na/au kabla na baada ya shule.

**Wizi/Umiliki wa Mali Iliyoibiwa (kiwango cha 1-6)** Kuchukua kinyume cha sheria, kuiba au kumiliki pesa au mali.

**Tumbaku au Zana za Kuvutia Sigara (kiwango cha 2-3)** Kumiliki Tumbaku au Zana za Kuvutia Sigara kumepigwa marufuku. "Sera hii inajumuisha, lakini haijakomea kwa, bidhaa zote za tumbaku za sigara ya elektroniki, vifaa vya kuvutia sigara, mirija ya elektroniki, kalamu za tumbaku, kifaa cha kuwasilisha nikotini, n.k.

**Uwepo Usioidhinishwa/Kuingia bila Ruhusa/Kutangatanga (kiwango cha 1-5)** Kuwa katika au karibu na eneo lolote la shule wakati mwanafunzi hana sababu halali ya kuwa hapo; kitendo cha kukusanyika au kuzurura katika jengo la shule au kwenye mali ya shule bila ruhusa ya mfanyakazi. Hii inajumuisha pia uwepo usioidhinishwa kwenye mali yoyote ya shule au eneo la jamii wakati wa saa za shule wakati mwanafunzi amesafiri kwenda au kutoka jengo au shughuli ya Wilaya ya Shule za Lansing. Mwanafunzi yeyote aliyeondoshwa kwa muda au kufukuzwa shuleni amepigwa marufuku kuwepo kwenye rasilimali yoyote ya Wilaya ya Shule za Lansing.

**Ukiukaji wa Sheria za Jiji, Jimbo au Serikali, au Vitendo vya Jinai (kiwango cha 2-6)** Kuanzisha au kushiriki katika vitendo vyovyote vilivyopigwa marufuku na sheria ya serikali au jimbo au za ndani wakati vitendo kama hivyo vinaathiri usalama na shughuli za kawaida za shule, haijalishi kama kutakuwa na mashtaka ya jinai.

**Silaha (kiwango cha 2- 6)** Uuzaji, au Matumizi, kubeba, kutumia, kushughulikia, kuhifadhi au kutishia kwa kutumia silaha au vitu vingine hatari shuleni au kwenye uwanja wa shule kunaweza kusababisha mwanafunzi kuondoshwa kwa muda. Silaha zinafafanuliwa katika kategoria tatu (3): (1) silaha hatari ambazo zinahitaji kufukuzwa kabisa: (bunduki, dirk, daga, stileto, kisu chenye bapa zaidi ya inchi tatu (3), kisu kinachofunguliwa kwa mashine, mtalimbo, ngumi ya vyuma); (2) silaya nyingine zinazotumiwa sana au zilizoundwa kusababisha madhara ya kimwili au kutisha ikiwemo, lakini hazijakomea kwa: bunduki za hewa (bunduki za hewani zinaweza kuwa hatari, na ni tofauti na bunduki za airsoft), bunduki za bb, mijeledi, billy clubs, vigongo, vishtuaji, vifaa vinavyochomoa gesi, kisu chenye bapa ya inchi tatu (3) au chini kwa urefu, grunedi, minyororo, rungu na silaha za sanaa ya vita; (3) makala yaliyokusudiwa malengo mengine ambayo yanatumiwa kusababisha madhara ya kimwili au kutishia, ikiwemo lakini hayajakomea kwa: mikanda, vikata sanduku, vichana, penseli, faili, nyembe na dira.

## Kuondoshwa

Kumwondoa mwanafunzi shuleni kwa sababu za kinidhamu kwa kipindi cha **chini ya siku 60 za shule**.

Ukiukaji usiokithiri wa Mwongozo huu wa Mwanafunzi (angalia kurasa za unaweza kusababisha kuondolewa shuleni kwa muda. Walimu wakuu wa shule wanaweza kumwondoa mwanafunzi hadi siku 9 kwa ukiukaji wowote. Kuondoshwa kwa muda kutajumuishwa katika rekodi za mwanafunzi, kwa kutegemea hatua ya baadaye ya nidhamu kulingana na mtindo wa tabia. Kuondoshwa kokote kunaopendekezwa kwa zaidi ya siku 10 kunaweza kuhitaji kupelekwa kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule na nyaraka inayounga mkono mazingatio ya jimbo ya Vipengele 7 za kisheria.

Mwanafunzi aliyeondoshwa huenda asiwe kwenye rasilimali ya shule, kuhudhuria shughuli yoyote inayohusiana na shule au kushiriki katika shughuli yoyote ya shule ya baada ya masomo akiwa ameondoshwa, bila ruhusa ya mwalimu mkuu. Lazima shule itoe kazi ya elimu kwa mwanafunzi aliyeondoshwa wakati wa kipindi cha kuondoshwa. Ni wajibu wa mzazi kuwasiliana na shule kuhusu kupokea kazi kama hiyo ambayo itapatikana kwa mzazi saa 24 baada ya ombi kupokewa. Mara moja baada ya kurudi shule baada ya kuondoshwa, mwanafunzi atawajibika

kuwasiliana na mwalimu ili kuhakikisha kazi zote zilizokosekana za darasani zimekamilishwa. Mwalimu mkuu anaweza kuitisha mkutano na mzazi na mwalimu na, inapofaa, mwalimu kabla ya mwanafunzi kurejea. Lengo la mkutano huu ni kuunda mpango wa ufanisi wa mwanafunzi. Mpango utaandikwa, kutiwa saini na nakala kupewa mwanafunzi, mzazi na mwalimu, na hata pia kuwasilishwa shuleni.

## Kuondoshwa na Mwalimu Darasani

Ijapokuwa "Kuondoshwa Darasani" ni sehemu ya sheria ya Jumla ya Michigan, tunaamini haipaswi kutumiwa sana, hiyo ni hata kama itatumika. Mwalimu anaweza kumwondosha mwanafunzi kutoka kwa darasa la mwalimu kwa hadi siku moja ikiwa tabia ya mwanafunzi inazidisha viwango vilivyofafanuliwa na sera ya ndani. Sera hii itatumiwa kama sehemu ya Kanuni ya Maadili Mema ya wilaya ya shule na itaelezea aina za tabia ambazo mwanafunzi anaweza kufukuziwa. Ikiwa mwanafunzi atasalia shuleni, lazima asimamiwe ipasavyo. Sheria inahitaji mwalimu anayetumia chaguo hili aripoti "Kuondoshwa Darasani" kwa ofisi, kisha, kwa haraka iwezekanavyo, apange mkutano na wazazi au walezi wa mwanafunzi aliyeondoshwa na ajaribu kumhusisha mshauri wa shule, mhudumu wa jamii, au mwanasaikolojia. Ikiwa mwalimu au mzazi ataomba kwamba msimamizi wa shule ahudhurie, lazima mwalimu amhusishe pia msimamizi katika mkutano huo. Mwanafunzi anaweza kurudi siku hiyo ya shule darasani, kwa masomo, au shughuli ambayo aliondolewa, kwa maelewano na mwalimu mkuu wa shule [MCL 380.1309]. Chanzo: Kanuni za Maadili Mema ya Modeli ya MDE.

## Mwongozo wa Kuondoshwa Darasani

Watu wanaostahiki kutumia kuondoshwa darasani wanajumuisha walimu katika Wilaya ya Shule ya Lansing ambao wanahusika na darasa, somo au shughuli.

Katika kiwango cha msingi, darasa, somo au shughuli hufafanuliwa kama kipindi cha muda ambacho mwalimu anahusika moja kwa moja kutoa mafunzo au usimamizi. Katika kiwango cha sekondari, darasa, somo, au shughuli hufafanuliwa kama kipindi cha wakati ndani ya ratiba ya mwanafunzi ambayo mwalimu ana jukumu la moja kwa moja la kutoa mafunzo au usimamizi.

Ikiwa mwalimu ataondosha mwanafunzi, lazima mwalimu aripoti uondoshaji wake na sababu ya kuondoshwa kwa mwalimu mkuu katika maandishi kwa haraka iwezekanavyo kama majukumu ya kufundisha inaruhusu, lakini hakuna kesi baadaye mwisho wa siku ya mwalimu, kwa kutumia fomu ya mwanafunzi kuondoshwa. Lazima mwalimu ampeleke mwanafunzi kwa mwalimu mkuu kuchukua hatua inayofaa. Mwanafunzi akiendelea kuwa shuleni, mkuu wa shule atahakikisha kwamba mwanafunzi atakuwa chini ya uangalizi unaofaa. Mwanafunzi hatarudishwa siku hiyo ya shule kwa darasa, somo au shughuli ambayo aliondoshwa bila makubaliano ya pamoja ya mwalimu anayeondosha na mwalimu mkuu. Kuondoshwa darasani kunaweza kuwa kwa siku moja kamili ya shule katika kiwango cha msingi au kipindi kimoja kamili cha darasa katika kiwango cha sekondari.

Mapema iwezekanavyo baada ya kuondoshwa darasani, lakini sio zaidi ya siku ya shule inayofuata, mwalimu atamwomba mzazi wa mwanafunzi ahudhurie mkutano wa wazazi na mwalimu kujadili kuondoshwa. Mwalimu ataripoti matokeo ya mkutano huo kwa mkuu wa shule katika maandishi kabla ya siku inayofuata ya shule kwa kutumia fomu ya ripoti ya mkutano wa wazazi na mwalimu. Wakati wowote inapowezekana, mshauri wa shule, mwanasaikolojia au mfanyakazi wa jamii atahudhuria mkutano huo. Mwalimu mkuu atahudhuria mkutano iwapo mwalimu au mzazi ataomba.

## Kupelekwa kwenye Ofisi ya Utamaduni wa Shule

Matukio yote ya kuondolewa shuleni yanayopendekezwa kwa siku 10 au zaidi yanapaswa kupelekwa kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule na yanahitaji mkuu wa shule au mwakilishi atoe hati zinazounga mkono sheria ya serikali ya Kuzingatia Mambo 7 ya Lazima (Mandatory 7 Factors Consideration). Ripoti ya Idara ya Usalama wa Umma inahitajika kupelekwa kwenye Ofisi ya Utamaduni wa Shule.

Itakuwa jukumu la mkuu wa shule kupanga mkutano na Ofisi ya Utamaduni wa Shule mwishoni mwa siku inayofuata ya shule. Mkuu wa shule atamjulisha mzazi kuhusu wakati, tarehe na eneo la mkutano. Mwalimu mkuu atashiriki katika mkutano huo na mwanafunzi na mzazi, kila inapowezekana na atatekeleza uamuzi uliotolewa na Ofisi ya Utamaduni wa Shule.

## Kufukuzwa

Kufukuza mwanafunzi shuleni kwa sababu za kinidhamu kwa kipindi cha **siku 60 au zaidi za shule**.

Ukiukaji mkubwa wa Kijitabu cha Wanafunzi (tazama kurasa 28-32) unaweza kusababisha kufukuzwa kutoka kwa wilaya ya shule. Bodi ya Elimu au mwakilishi wake hutoa uamuzi wa mwisho wa kufukuzwa. Kufukuzwa chini mamlaka ya serikali kutaamuliwa na wanachama wa Halmashauri ya Elimu na uamuzi wao ni wa mwisho. Kufukuzwa yote isiyo ya lazima kutaamuliwa na Timu ya Ushauri iliyoteuliwa na Halmashauri ya Elimu.

### Kufukuzwa Kulikoamrishwa na Jimbo

(Kijitabu cha Shule Kilichopitiwa 380.1311)

Sheria ya serikali inapendekeza Halmashauri ya Elimu au mwakilishi wake azingatie kufukuzwa kabisa, chini ya uwezekano wa kurudishwa na Halmashauri ya Elimu, kwa mwanafunzi yeyote ambaye:

1. Anamiliki silaha hatari (silaha ya moto, hanjari, kisu na wembe zaidi ya inchi tatu [3] kwa urefu, kisu cha mfukoni kilichofunguliwa na kifaa cha mitambo, chuma, au konzi ya shaba) katika eneo la shule lisilo na silaha;
2. Anaanzisha moto kwa makusudi katika majengo ya shule au kwenye uwanja wa shule;
3. Anafanya tabia ya kingoni ya jinai katika majengo ya shule au kwenye uwanja wa shule;
4. Anafanya (katika gredi ya sita au zaidi) shambulio la kimwili dhidi ya mfanyakazi wa shule, anayejtolea, au kontrakta kwenye eneo la shule, au gari la shule, au kwenye shughuli inayofadhiliwa na shule, bila kujali eneo.

Sheria ya serikali inapendekeza mwanafunzi afukuzwe kwa muda wa chini uliobainishwa hapa chini kabla ya kurudishwa:

1. Silaha hatari (gredi ya sita au zaidi): kufukuzwa kabisa
2. Silaha hatari (gredi ya tano au chini):
    - Siku tisini (90) za shule ikiwa bunduki au silaha inatumiwa kutishia mtu mwingine
    - Siku kumi (10) za shule ikiwa sio bunduki au ikiwa haitumiwi kumtishia mtu mwingine
3. Shambulio la kimwili kwa mfanyakazi au anayejitolea:
    - Wanafunzi wa gredi ya sita na zaidi: kufukuzwa kabisa
    - Wanafunzi wa gredi ya tano na chini: uamuzi wa Halmashauri ya Elimu na mwakilishi
4. Mwenendo wa Kingono wa Jinai ambayo inastahiki kama uhalifu chini ya Kanuni ya Adhabu ya Michigan: Siku mia moja themanini (180)
5. Uchomaji kwa makusudi: Siku mia moja themanini (180)
6. Mapendekezo ya kumfukuza kabisa mwanafunzi yatawasilishwa na Msimamizi wa Shule kwa Halmashauri ya Elimu na mwakilishi ndani ya siku thelathini (30) za shule baada ya kuondoshwa kulingana na uchunguzi wa tukio hilo uliofanywa na afisa husika wa usalama wa shule na/au Wafanyakazi wa kituo wa Idara ya Usalama wa Umma. Iwapo mambo yaliyopo yatatokea, Msimamizi atakuwa na siku kumi (10) za ziada za shule ambazo ataleta mapendekezo ya kufukuzwa kwa Halmashauri.

## Mambo ya Lazima ya Kuzingatia

(Kijitabu cha Shule Kilichopitiwa 380.1310d [4])

Isipokuwa kwa matumizi/umiliki wa silaha, ni lazima kuzingatia mambo yafuatayo

kabla ya kuondosha au kumfukuza mwanafunzi kwa siku 10 au zaidi za shule:

1. Umri wa Wanafunzi
2. Historia ya Nidhamu
3. Hali ya Ulemavu
4. Ukali wa Tabia
5. Ikiwa tabia hiyo ilikuwa na hatari ya usalama
6. Ikiwa haki ya kurejesha maadili inaweza kubadilisha tabia au la
7. Ikiwa uingiliaji mdogo utashughulikia tabia hiyo au la

Shule zitazingatia kutumia taratibu za kurejesha maadili kama njia mbadala ya kuondoshwa au kufukuzwa. Shule ikiondosha au kumfukuza mwanafunzi, shule itazingatia kutumia taratibu za kurejesha maadili pamoja na kuondoshwa au kufukuzwa.

**Dhana Inayoweza Kurejelewa**

Dhana kwamba kuondoshwa hakujathibitishwa isipokuwa mambo 1310d yatazingatiwa. Dhana inayoweza kurejelewa ni moja ambayo inaweza kushinda ikiwa ushahidi unaonyesha kuwa dhana hiyo sio sahihi.

Katika kuondoshwa kwa siku 9 au chini, hakuna dhana inayoweza kurejelewa, lakini shule itazingatia kila moja ya mambo yaliyo hapa juu kutoa uamuzi.

**Kikwazo kimoja**

Mwanafunzi anayemiliki silaha (isipokuwa bunduki) anaweza kuanzisha moja ya yafuatayo kwa njia wazi na ya kuridhisha:

1. Silaha haikukusudiwa kutumiwa kama silaha, au kwa uwasilishaji wa matumizi kama silaha;

2. Silaha hiyo ilimilikiwa bila kujua;

3. Mwanafunzi hakujua kifaa hicho kilizingatiwa kuwa silaha;

4. Silaha hiyo ilimilikiwa kwa pendekezo, ombi au idhini ya wafanyakazi wa shule, DPS, au polisi

Dhana Inayoweza Kurejelewa ya Silaha:

- Halmashauri AU mwakilishi huamua katika maandishi kwamba angalau moja ya ruhusa ya silaha imeanzishwa kwa njia wazi na ya kuridhisha NA

- Mwanafunzi hana historia ya kuondoshwa au kufukuzwa

Wilaya ya Shule ya Lansing inaweza kutumia busara kwa kuzingatia kuondoshwa kwa zaidi ya siku 10 au kufukuzwa. Hata hivyo, kutakuwa na dhana inayoweza kurejelewa (dhana kwamba kuondoshwa sio lazima kulingana na ushahidi) kwamba kuondoshwa hakuruhusiwi isipokuwa (shule) inaweza kuonyesha kila moja ya mambo yaliyo hapo juu.

## Kuondoshwa kwa Muda Kusio kwa Lazima

Kama inavyopendekezwa na Sheria ya Jimbo, Halmashauri au mwakilishi anaweza kuondosha au kufukuza, chini ya uwezekano wa kurudishwa, mwanafunzi katika gredi ya 6-12 ambaye:

1. Anatoa tishio la bomu au tishio kama hilo linaloelekezwa kwa majengo ya shule, mali nyingine ya shule au matukio yanayohusiana na shule.

2. Anafanya shambulio la kimwili dhidi ya mwanafunzi mwingine kwenye eneo la shule, au katika gari la shule, au kwenye shughuli inayofadhiliwa na shule, bila kujali eneo.

Tabia yoyote, gredi ya K-12, ambayo inatishia usalama wa wanafunzi na au wafanyakazi wa Wilaya ya Shule ya Lansing inaweza kusababisha kufukuzwa.

Inapofaa, wanafunzi waliofukuzwa wataelekezwa kwa mashtaka. Wanafunzi ambao wanaamini kuwa ni waathirika wa mwenendo wa kingono wa jinai wanaweza (1) kuwasilisha malalamiko rasmi au yasiyo rasmi na Maafisa wa Wilaya wa Utekelezaji Sheria (tazama ukurasa wa 6); (2) anaweza kuwasilisha malalamiko ya jinai kwa wakala wa kutekeleza sheria; au (3) kufuata aina zote mbili za malalamiko, kwa wati mmoja.

# Taratibu za Rufaa

## Kuondolewa kwa Kiwango cha Shule

1. Mzazi wa mwanafunzi aliye chini ya umri wa miaka 18 au mwanafunzi (ikiwa ana miaka 18) atakata rufaa kwanza hatua ya kinidhamu kwa msimamizi aliyeweka adhabu hiyo.
2. Katika kiwango cha sekondari, rufaa zaidi inaweza kuelekezwa kwa mwalimu mkuu.
3. Rufaa zaidi ya kiwango cha shule zitaelekezwa kwa Msimamizi wa Shule au yule mwakilishi wao.
4. Rufaa zote kutoka nje ya Lansing School District zinahitaji kuelekezwa kwa Msimamizi.

## Maamuzi ya Ofisi ya Utamaduni wa Shule

1. Mzazi wa mwanafunzi aliye chini ya umri wa miaka 18 au mwanafunzi (ikiwa ana miaka 18) ataomba fomu ya rufaa kutoka kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule.
2. Lazima fomu ya rufaa irudishwe kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule ndani ya siku tano (5) za shule baada ya kupokea uamuzi katika maandishi.
3. Msimamizi Mtendaji wa Utamaduni na Mazingira ya Shule (School Culture and Climate) ataitisha mkutano ndani ya siku kumi (10) za shule baada ya ombi kuwasilishwa ili kusikiliza rufaa hiyo.

## Maamuzi ya Timu ya Ushauri

1. Mzazi wa mwanafunzi aliye chini ya umri wa miaka 18 au mwanafunzi (ikiwa ana miaka 18) ataomba fomu ya rufaa kutoka kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule.
2. Lazima fomu ya rufaa irudishwe kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule ndani ya siku tano (5) za shule baada ya kupokea uamuzi katika maandishi.
3. Timu ya Ushauri itaitisha usikilizaji ndani ya siku kumi (10) za shule baada ya ombi, ikiwa imewasilishwa.
4. Mzazi wa mwanafunzi aliye chini ya umri wa miaka 18 au mwanafunzi (ikiwa ana miaka 18) atapokea taarifa ya uamuzi kutoka kwa Timu ya Ushauri wa Kufukuzwa.

Timu ya Ushauri ni waakillishi wa Halmashauri ya Elimu; kwa hivyo uamuzi wa rufaa ni wa mwisho. Hakuna mchakato zaidi wa rufaa kwa uamuzi huu. Maamuzi ya kufukuzwa kwa lazima kunakoamuliwa na Halmashauri ya Elimu ya Shule ya Lansing ni ya mwisho na hakuna mchakato wa rufaa.

# Kurejeshwa

Mwanafunzi aliyefukuzwa kabisa anaweza kuomba kurejeshwa kwa Halmashauri ya Elimu kama inaruhusiwa na sheria. Mwanafunzi mwingine yeyote aliyefukuzwa atarejeshwa chini ya hali ya kuandikishwa tena. Masharti haya ni kama yafuatayo:

1. Taarifa, iliyotolewa na mzazi, kutoka kwa mshauri mwenye leseni, ikisema kuwa mwanafunzi ameshiriki katika kiwango cha chini cha vikao sita (6) vya ushauri na inapendekezwa arudi kwenye mpango wa kawaida wa shule.
2. Taarifa iliyoandikwa, iliyotolewa na mwanafunzi, inayoonyesha ako tayari kufuata sheria na kanuni zote za Kijitabu cha Wanafunzi.
3. Taarifa kutoka kwa mamlaka ya utekelezaji wa sheria ya ndani, iliyotolewa na Huduma za Wanafunzi, ikionyesha kwamba hakukuwa na mawasiliano yoyote mabaya na watekelezaji wa sheria.
4. Uthibitishaji, uliotolewa na Huduma za Wanafunzi, kwamba mwanafunzi huyo hajapatikana akiingia bila ruhusa katika Wilaya ya Shule ya Lansing wakati wa kipindi chake cha kufukuzwa.
5. Uthibitishaji, uliotolewa na Ofisi ya Utamaduni wa Shule, ya kushiriki katika Ushirikiano wa Kuhitimu kwa wanafunzi ambao ni kati ya umri wa miaka 14-19.

Kukamilisha kwa kuridhisha kwa vigezo vilivyo hapo juu hakutasababisha kuandikishwa tena kwa moja kwa moja, lakini itatumika kama kiwango cha chini cha juhudi na tabia ambayo mwanafunzi lazima aonyeshe katika ombi la kuandikishwa tena.  Masharti ya ziada yanaweza kuwekwa, kama inavyohitajika kwa hali ya mtu binafsi.



* Hali ya nidhamu ya mwanafunzi itabaki vile vile katika taratibu za rufaa.

# Mwongozo wa Nidhamu

## Hali ya Nidhamu

Asili ya nidhamu inamaanisha kila mtu anayehusika katika mchakato kukubali haki na majukumu na: mwanafunzi, mzazi, mwalimu, msimamizi na wafanyakazi wengine wote wa shule. Wakati Msimamizi wa Shule ana jukumu la msingi la kudumisha udhibiti na nidhamu inayofaa ndani ya majengo na viwanja vya shule, kila mwalimu ana jukumu la msingi la kudumisha udhibiti na nidhamu inayofaa ndani ya darasa. Walimu pia hushiriki jukumu la kudumisha udhibiti na nidhamu inayofaa katika maeneo mengine ya majengo na viwanja vya shule. Hatua na mbinu za kinidhamu zitakuwa za busara, za haki, za haraka na kulingana na sera na taratibu za Mwongozo wa Wanafunzi wa Lansing School District.

Wilaya ya Shule ya Lansing inatambua kuwa wazazi ni sehemu muhimu ya elimu ya mtoto wao, ambayo inajumuisha tabia shuleni. Kwa hivyo, ili kuendelea kuwajulisha wazazi, waalimu na wafanyakazi wengine watawasiliana na wazazi kuhakikisha wanafahamu kuhusu maswala ya tabia. Matokeo chanya ya maendeleo yanapaswa kuungwa mkono na uingiliaji mzuri wa maendeleo.

### Kiwango cha 1: *Hatua Zinazoelekezwa na Walimu/Wafanyakazi*

Walimu/timu/wafanyakazi wanaweza kuanzisha hatua zozote zifuatazo:

1. Kutunga sheria/matarajio na athari dhahiri za darasani kama jamii kulingana na matarajio ya shule nzima na kuzitekeleza kwa uaminifu
2. Kutuza tabia zinazofaa
3. Tambua na uthawabishe tabia inayofaa ya wanafunzi wote
4. Rufaa kwa msimamizi wa kesi, timu ya usaidizi wa uingiliaji
5. Mawasiliano ya simu na mzazi (shiriki sehemu nzuri za ukuaji)
6. Barua kwa mzazi (shiriki mazuri na maeneo ya ukuaji)
7. Chumba cha kutulia: Mwanafunzi kuondolewa kwenye darasa kwa nusu ya siku au chini yake
8. Kuzuiwa: Kumzuia mwanafunzi kwa sababu za kinidhamu kabla, wakati au baada ya saa za shule
9. Shughuli Iliyozuiliwa: Kukatazwa kushiriki katika shughuli za shule na/au matukio ya masomo ya ziada (pamoja na mapumziko)
10. Huduma za jamii/shule: Mwanafunzi kuwekwa kufanya huduma za jamii/shule
11. Kuondolewa Darasani
12. Rufaa kwa mshauri wa shule, msimamizi wa kesi, timu ya usaidizi wa uingiliaji (Mtaalamu wa Ufikiaji wa Jamii, wafanyakazi wa jamii, Wataalamu wa Usaidizi wa Wanafunzi, Mawakili wa Wanafunzi, Wataalam wa Tabia), wafanyakazi wa mahudhurio, Watendaji wa Sheria ya Marejesho ya Maadili au wafanyakazi wengine
13. Mkataba wa Tabia au Mpango wa Mafanikio/Tabia na mwanafunzi/mzazi: Taarifa iliyoandikwa inayoorodhesha hatua na matokeo ya kuchukuliwa ili kuboresha tabia au mahudhurio
14. Kwa kushirikiana na mkuu wa shule, peleka kwa Timu ya Usuluhishi wa Matatizo/Uingiliaji wa Tabia: Mkutano wa wafanyakazi wa shule, wazazi, na watu wengine wa kuzingatia tabia na/au maendeleo ya mwanafunzi na kutoa mapendekezo
15. Chaguo nyingine kama ilivyojadiliwa kati ya wazazi, walimu na wasimamizi
16. Ishara zisizo za sauti za maelekezo
17. Onyo kwa matamshi
18. Mruhusu mwanafunzi atulie
19. Kurejelea, kufafanua na kuhimiza matarajio/makubaliano
20. Toa maagizo ya wazi
21. Badilisha matarajio panapohitajika
22. Kutafakari kuhusu matukio ya mwanafunzi (maandishi au sauti)

### Kiwango cha 2: *Hatua Zinazoelekezwa na Wasimamizi*

Mkutano wa msimamizi/mzazi/mwanafunzi lazima ufanyike na unaweza kutokea pamoja na moja au zaidi ya yafuatayo:

1. Arifa rasmi ya utoro iliyotumwa kwa wazazi
2. Rufaa kwa Mtaalam wa Sheria ya Kurejesha Maadili
3. Shule ya jumamosi/jioni: Mipango ya kuzuia ya Jumamosi au saa zingine zisizo za shule

4. Kuripotiwa kwenye ofisi DPS kwa ajili ya kuchukuliwa hatua
5. Chaguo zilizojadiliwa kati ya wazazi, walimu na wasimamizi, yaani huduma ya jamii, kurejesha, n.k.
6. Mwalimu mkuu au mwakilishi kutoa hati zinazounga mkono mazingatio ya kisheria ya vipengele 7, ambayo ni ya lazima
7. Kuripotiwa kwa Community Mental Health-ACCESS kwa ukaguzi wa matumizi ya dawa za kulevya au wa afya ya akili.
8. Lugha ya hisia
9. Matarajio ya ukaguzi
10. Kupokonywa kifaa kinachosababisha usumbufu kwa muda mfupi na kuruhusu mwanafunzi kutafakari kuhusu matarajio na kujua ni kwa nini kifaa kilichukuliwa kwa kutumia lugha ya hisia
11. Kuandika au kurekodi msamaha kwa kila mtu aliyeathiriwa na vitendo
12. Rekodi ya kutafakari iliyoandikwa
13. Kuondolewa kwa muda darasani na mazungumzo ya ghafla ya marekebisho
14. Mtu mzima mshauri (usaidizi kwa siku 10-30 kwa kuhudhuria)
15. Kuungana na mtu mzima kwa kuhudhuria na kuondoka (siku 10)
16. "Hati ya Kutafakari" yenye maswali ya marekebisho
17. Kusuluhisha matatizo kwa njia ya marekebisho
18. Maankuli kimya

## Kiwango cha 3: *Shule Mbadala*

1. Mwanafunzi kuwekwa katika mpango mbadala wa shuleni
2. Uwekaji (katika kitone cha 1) pamoja na matokeo ya kiwango cha 1 na 2
3. Mabadiliko katika kazi ya darasa
4. Mpango wa kurekebisha tabia na huduma ya jamii inayohusiana na shule
5. Mpango wa tabia na mwanafunzi/mzazi: Taarifa iliyoandikwa inayoorodhesha hatua na matokeo ya kuchukuliwa. Taarifa hiyo pia inaelezea usaidizi utakaotolewa na wafanyakazi wa shule na/au mzazi pamoja na tarehe ambayo mpango ulikaguliwa
6. Kuripotiwa kwenye ofisi ya taratibu za haki ya urejeshaji kupitia mkataba uliokamilika na wahusika wote
7. Kuripotiwa kwa wahudumu wa masuala ya tabia
8. Kuripotiwa kwa Timu ya Huduma za Wanafunzi/Masuala ya Tabia (Student Services Team/Behavior Intervention Team)

## Kiwango cha 4: *Kuondoshwa kwa Muda Shuleni (Hadi na Ikiwemo Siku 9)**

Kuondoshwa chini ya mkutano wa wazazi na mpango wa kuandikishwa tena, ambao lazima ujumuishe uingiliaji kutoka kwa Viwango vya 1-3 inapofaa.

## Kiwango cha 5: *Matokeo/Mipango Mbadala**

1. Mpango wa kurekebisha tabia na ratiba maalum kwa idhini ya Usimamizi Mkuu.
2. Mpango wa kurekebisha tabia unaweza kuwa pamoja na matokeo ya Viwango 2,3,4
3. Ushauri wa Ofisi ya Utamaduni wa Shule
4. Uhamisho wa Usimamizi
5. Kuripotiwa kwa mipango mbadala
6. Kwa tukio la kufukuzwa shuleni kwa siku 10 au zaidi, hati zinazounga kigezo cha 7 cha sheria ya jimbo ni **lazima zitumiwe**

## Kiwango cha 6: *Mkutano wa Kufukuzwa/Kufukuzwa**

Kufukuzwa ni mwanafunzi kunywimwa haki ya kuhudhuria shule au shughuli zilizofadhiliwa na shule.

- Pendekezo la kuondoshwa kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule kuzingatia kufukuzwa, kwa kuzingatia vipengee 7.

*Lazima msimamizi awasiliane na mzazi/mlezi na afanye mipangilio ya kutoa kazi/mitihani ya kila siku au kila wiki za mwanafunzi.

## Maafisa wa Wilaya wa Utekelezaji

**Darin Walter**
*Mratibu wa Title IX*
darin.walter@lansingschools.net
517-755-2037

**Erin Miracle**
*Afisa wa Kufuatilia Title IX*
erin.miracle@lansingschools.net
517-755-2010

# Hatua za Kinidhamu za K-8

| TABIA ZINAZOSABABISHA UINGILIAJI | RIPOTI YA DIPS INAHITAJIKA | MAKOSA MADOGO MIKAKATI YENYE SAFU | KIWANGO CHA MARUDIO MIKAKATI YENYE SAFU | UINGILIAJI MKUBWA WENYE SAFU* |
|---|---|---|---|---|
| **Lugha ya Matusi** | Hapana | 1-2 | 1-4 | - |
| **Pombe** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| ***Uchomaji kwa Makusudi** | Ndiyo - wasiliana na Wazima Moto | - | - | 5-6 |
| **Shambulio kwa Wafanyikazi (Kimwili)** | Ndiyo - ikiwa inapelekwa kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule au inahusisha jeraha | 1-2 | 2-4 | 5-6 |
| **Shambulio kwa Mwanafunzi (Kimwili)** | Ndiyo - ikiwa inapelekwa kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule au inahusisha jeraha Uingiliaji unapaswa kuandikwa katika Synergy. | 1-2 | 2-4 | 5-6 |
| **Tishio la Bomu - Tishio Dhidi ya Shule** | Ndiyo | 2-3 | 2-3 | 4-5 |
| **Udhalimu** | Ndiyo - Wakati tabia inarudiwa au kuondoshwa na Ofisi ya Utamaduni wa Shule | 1-2 | 2-4 | 5-6 |
| **Kudanganya/Uigaji** | Hapana | 1-3 | 2-4 | - |
| **Tabia Isiyofaa** | Hapana | 1-2 | 2-4 | 5 |
| **Vifaa vya Mawasiliano ya Kielektroniki (ECD)** | Hapana - isipokuwa kuondoshwa na Ofisi ya Utamaduni wa Shule | 1-2 | 2-4 | 5 |
| **Vilipuzi/Vifaa vya Kuchoma Kuuza, Kumiliki au Kutumia** | Ndiyo | 1-2 | 2-4 | 5-6 |
| **Uporaji/Wizi** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| **Kengele/Simu za 911 za Uongo** | Ndiyo | - | 2-4 | 5 |
| **Kupigana** | **Mapigano ya kwanza na ya pili:** Hapana<br>**Mapigano yanayofuata:** Ndiyo | 2-3 | 2-4 | 5-6 |
| **Kughushi** | Hapana | 1-2 | 1-4 | - |
| **Kucheza kamari** | Hapana | 1-3 | 1-4 | - |
| **Shughuli za Magenge** | Ndiyo | 1-3 | 1-4 | 5 |
| **Udhalilishaji** | Hapana | 1-3 | 1-4 | - |
| **Kukosa kutii** | Hapana | 1-2 | 1-4 | - |
| **Kuogofya/Kufuata/Vitisho kwa Wanafunzi** | Ndiyo | 1-3 | 2-4 | 5-6 |
| **Uharibifu Mbaya** | Hapana - isipokuwa hali hiyo inahusisha mali yenye thamani ya $200+ | 1-2 | 2-4 | 5 |
| **Bangi na Dawa Zingine Zinazodhibitiwa** | Ndiyo | - | 2-4 | 5 |
| **Tabia Chafu** | Hapana - isipokuwa kuondoshwa na Ofisi ya Utamaduni wa Shule | 1-3 | 2-4 | 5 |
| **Umiliki/Matumizi ya Kitu Kinachofanana Bunduki/Kifaa cha Kucheza au Picha** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| **Umiliki/Matumizi ya Bunduki ya Airsoft** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| ***Kuuza/Kusambaza Dawa za Kulevya au Pombe** | Ndiyo | - | - | 5-6 |
| ***Hujumu ya kingono** | Ndiyo | - | - | 5-6 |
| **Kutuma Ujumbe Mchafu/Ponografia ya Watoto** | Ndiyo | 1-3 | 2-4 | 5-6 |
| **Unyanyasaji wa Kingono** | Ndiyo | 1-3 | 2-4 | 5 |
| **Wizi** | Hapana - isipokuwa hali hiyo inahusisha mali yenye thamani ya $200+ | 1-3 | 2-4 | 2-5 |
| **Tumbaku na Vifaa vya Kuvuta Moshi** | Hapana - isipokuwa ni kosa linalorudiwa | - | 2-4 | - |
| **Uwepo Usioidhinishwa/Kuingia Bila Ruhusa/ Kutangatanga** | Ndiyo - tumia onyo au barua ya kuingia bila ruhusa, mashtaka ya sheria yanatafutwa (ripoti kamili inahitajika) | 1-3 | 2-4 | - |
| **Ukiukaji wa Sheria za Jiji, Jimbo, au Sheria ya Shirikisho au Vitendo vya Jinai** | Ndiyo | 2-3 | 2-4 | 5-6 |
| ***Silaha - Kuuza, Kumiliki au Kutumia** | Ndiyo | 2-4 | 4 | 5-6 |

*Inahitaji kuondoshwa na Ofisi ya Utamaduni wa Shule.

| TABIA ZINAZOSABABISHA UINGILIAJI | RIPOTI YA DIPS INAHITAJIKA | MAKOSA MADOGO MIKAKATI YENYE SAFU | KIWANGO CHA MARUDIO MIKAKATI YENYE SAFU | UINGILIAJI MKUBWA WENYE SAFU* |
|---|---|---|---|---|
| **Lugha ya Matusi** | Hapana | 1-2 | 1-4 | - |
| **Pombe** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| ***Uchomaji kwa Makusudi** | Ndiyo - wasiliana na Wazima Moto | - | - | 5-6 |
| **Shambulio kwa Wafanyikazi (Kimwili)** | Ndiyo | - | - | 5-6 |
| **Shambulio kwa Mwanafunzi (Kimwili)** | Ndiyo. Uingiliaji unapaswa kuandikwa katika Synergy. | - | 2-4 | 4-6 |
| **Tishio la Bomu - Tishio Dhidi ya Shule** | Ndiyo | - | - | 5-6 |
| **Udhalimu** | Ndiyo - wakati tabia inarudiwa au kuondoshwa na Ofisi ya Utamaduni wa Shule | 1-2 | 2-4 | 5-6 |
| **Kudanganya/Uigaji** | Hapana | 1-3 | 3-4 | - |
| **Dawa Zinazodhibitiwa au Dawa Zingine** | Ndiyo | - | 2-4 | 5 |
| **Tabia Isiyofaa** | Hapana | 1 | 1-4 | 5 |
| **Vifaa vya Mawasiliano ya Kielektroniki (ECD)** | Hapana | 1-3 | 2-4 | 5 |
| **Vilipuzi/Vifaa vya Kuchoma Kuuza, Kumiliki au Kutumia** | Ndiyo | 1-2 | 2-4 | 5-6 |
| **Uporaji/Wizi** | Ndiyo | - | 4 | 5-6 |
| **Kengele/Simu za 911 za Uongo** | Ndiyo - wasiliana na Wazima Moto | - | 4 | 5-6 |
| **Kupigana** | Ndiyo | - | **3-4**<br>**Kupigana mara ya kwanza na mara ya pili** kufukuzwa kwa siku 3 hadi 9 | 5-6<br>**Mapigano Yanayofuata*** |
| **Kughushi** | Hapana | 1-3 | 1-4 | - |
| **Kucheza kamari** | Hapana | 1-3 | 1-4 | 5 |
| **Shughuli za Magenge** | Ndiyo | 1-3 | 1-4 | 5-6 |
| **Udhalilishaji** | Hapana - isipokuwa kuondoshwa na Huduma za Wanafunzi | 1-3 | 4 | 5-6 |
| **Kukosa kutii** | Hapana | 1-3 | 1-4 | - |
| **Kuogofya/Kufuata/Vitisho kwa Wanafunzi** | Ndiyo | - | 1-4 | 5-6 |
| **Uharibifu Mbaya** | Hapana - isipokuwa hali hiyo inahusisha mali yenye thamani ya $200+ | 1-3 | 2-4 | 5 |
| **Bangi na Dawa Zinazodhibitiwa** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| **Tabia Chafu** | Ndiyo | 1-3 | 2-4 | 5 |
| **Umiliki/Matumizi ya Kitu Kinachofanana Bunduki/Kifaa cha Kucheza au Picha** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| **Umiliki/Matumizi ya Bunduki ya Airsoft** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| ***Kuuza/Kusambaza Dawa za Kulevya au Pombe** | Ndiyo | - | - | 5-6 |
| ***Hujumu ya kingono** | Ndiyo | - | - | 5-6 |
| **Kutuma Ujumbe Mchafu/Ponografia ya Watoto** | Ndiyo | - | 2-4 | 5-6 |
| **Unyanyasaji wa Kingono** | Ndiyo | 1-3 | 2-4 | 5 |
| **Wizi** | Hapana - isipokuwa hali hiyo inahusisha mali yenye thamani ya $200+ | 1-2 | 2-4 | - |
| **Tumbaku na Vifaa vya Kuvuta Moshi** | Hapana - isipokuwa ni kosa linalorudiwa | - | 2-4 | - |
| **Uwepo Usioidhinishwa/Kuingia Bila Ruhusa/ Kutangatanga** | Ndiyo - Iwapo mashtaka ya uhalifu yanapatikana au barua za onyo la kuingia bila ruhusa zinatumwa kwenye makazi . | 1-2 | 2-4 | - |
| **Ukiukaji wa Sheria za Jiji, Jimbo, au Sheria ya Shirikisho au Vitendo vya Jinai** | Ndiyo | 2-3 | 2-4 | 5-6 |
| ***Silaha - Kuuza, Kumiliki au Kutumia** | Ndiyo | - | - | 5-6 |

# Hatua za Kinidhamu za 6-12

*Inahitaji kuondoshwa na Ofisi ya Utamaduni wa Shule.

# Nidhamu kwa Wanafunzi walio na Mipango ya IEP na 504

Wanafunzi wenye ulemavu ambao wana Mipango ya Elimu za Kibinafsi (IEP) wana haki za ziada ulinzi wa taratibu kuhusu nidhamu. Hoja zilizo hapa chini hazitumiwi badala ya ilani kamili ya ulinzi wa taratibu ambayo inaweza kupatikana hapa: https://www.lansingschools.net/downloads/special_education/procedural_safeguards_notice_550307_7.pdf

1. Wanafunzi walio na IEPs wanaweza kuadhibiwa hadi siku 10 za shule. Huduma za elimu zinaweza kutolewa kwa mwanafunzi, ikiwa wilaya itatoa huduma kwa wanafunzi wote ambao wameondolewa pia.

2. Kabla ya kuondoshwa, lazima shirika linaloondosha lizingatie mambo yaliyoainishwa katika Kanuni ya Shule Iliyopitiwa katika 380.1310 (d).

3. Wakati mwanafunzi aliye na IEP ameondoshwa kwa zaidi ya siku 10, tarehe ambayo shule inatoa uamuzi wa kuondoshwa ambao ni mabadiliko ya mpango wa mtoto kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni za mienendo ya mwanafunzi, wilaya ya shule lazima iwajulishe wazazi kuhusu uamuzi huo, na iwape wazazi ilani ya ulinzi wa taratibu. Mwanafunzi basi ana haki ya Ukaguzi wa Uamuzi wa Udhihirisho (MDR). Uondoshaji wowote baadaye unaweza kuhitaji MDR.

4. Lazima MDR ikamilishwe na wazazi/walezi, wafanyakazi wa shule, na washiriki husika wa timu ya IEP ya mwanafunzi ndani ya siku 10 za shule kutoka tarehe ya uamuzi wa kubadilisha uwekaji wa mwanafunzi.

5. Kuondoshwa kwa muda darasani hakungeweza kuzingatiwa kama sehemu ya siku za kufukuzwa maadamu mwanafunzi amepewa fursa ya kuendelea vizuri katika mtaala wa jumla, kuendelea kupata huduma zilizoainishwa kwenye IEP ya mwanafunzi, na kuendelea kushiriki na wanafunzi wasio na ulemavu kwa kiwango ambacho wangekuwa nacho katika uwekaji wao wa sasa.

6. Katika hali ambapo mwanafunzi anaweza kuondoshwa kwa zaidi ya siku 10, mashauriano na Idara ya Elimu Maalum inahamasishwa.

Tafadhali angalia mchakato wa nidhamu kwa wanafunzi walio na IEP au mipango 504 waliopelekwa katika utaratibu wa Ofisi ya Utamaduni ya Shule kwenye ukurasa ufuatao kupata maelezo zaidi.



Mwanafunzi aliye na mpango wa IEP au 504 amekiuka kanuni ya maadili mema ya mwanafunzi. Tabia ya mwanafunzi haikuwa dhihirisho la ulemavu wa mwanafunzi na mwanafunzi huyo alipelekwa kwa Ofisi ya Utamaduni wa Shule (OSC).

Baada ya mkutano wa familia, OSC hufanya ukaguzi wa kesi ili iwasilishe kwa Mkurugenzi Mtendaji kwa ajili ya majadiliano na uamuzi wa hatua zinazofuata, ambazo zinajumuisha kurudi shuleni mara moja, kufukuzwa kwa muda mrefu, au kupelekwa kwa Timu ya Ushauri.

Kesi hukaguliwa na wafanyakazi wa OSC na kuandaa mkutano wa wazazi.

Mwanafunzi hupelekwa kwa Timu ya Ushauri, ambayo ni sehemu ya Halmashauri ya Elimu ya Shule ya Lansing. Madhumuni ya Timu ya Ushauri (CT) ni kutoa maamuzi ya nidhamu au uingiliaji kwa wanafunzi wanaokiuka Kijitabu cha Wanafunzi. Ukiukaji huu ni ukiukaji mbaya zaidi na unaopita kiasi.

Timu ya Ushauri iliamua mwanafunzi apate hatua zaidi za kinidhamu, hadi na ikiwezekana, kufukuzwa.

Mwanafunzi lazima akamilishe hali zinazohitajika kabla ya kurejesha kulingana na Sera ya Bodi 5610.

Mzazi huarifiwa kuhusu uamuzi wa Timu ya Ushauri na masharti ya kurejeshwa.

Mzazi anahakikisha kuwa masharti ya kurejeshwa yanatimizwa na kuwasilisha ombi la kurejeshwa.

OSC hukagua maombi ya kurejeshwa na inathibitisha masharti yametimizwa kwa mwanafunzi kurejea shuleni.

Wanachama wa Idara ya Mafundisho, Timu ya Utendaji, Msimamizi, au Halmashauri ya Elimu, wanaweza, inapohitajika, kutoa mwongozo wa hatua zinazofuata kuelekea kurejeshwa.

Timu ya Ushauri iliamua Mwanafunzi ASIPATE hatua za ziada za kinidhamu.

Mwanafunzi anarejea kwenye uwekaji wa shule. Masharti yanaweza kuwekwa wakati Mwanafunzi anarejea.

Mzazi na/au Mwanafunzi anaweza kuwasiliana na OSC wakati wowote kuuliza maswali au kupata habari za hali kuhusu mchakato.

Ikiwa Mzazi hajawasiliana na OSC siku kumi kabla ya tarehe ya kurejeshwa, OSC itawasiliana na Mzazi ili kujua ustahiki wa Mwanafunzi kurejeshwa.

Ikiwa Mwanafunzi hakutimiza masharti ya kurejea, OSC huamua sababu ya kutoweza kutimiza masharti hayo, na inawashauri familia katika kutimiza masharti ya kurejeshwa.

Afisa Usikilizaji wa Timu ya Ushauri ataarifiwa na kushauriwa ili kuamua ikiwa kesi hiyo inahitaji kukaguliwa na Idara ya Mafundisho, Timu ya Utendaji, Msimamizi, au Halmashauri ya Elimu.

# Nyongeza

## Kanuni ya Maadili Mema ya Masomo ya Mtandaoni

Wanafunzi wa Capital Area K-12 wanaopata masomo ya mtandaoni wako chini ya sera sawa za wilaya katika Kanuni za Maadili ya Wanafunzi na pia Kanuni ya Maadili ya Masomo ya Mtandaoni. Kuna sheria na matarajio ya ziada ya wanafunzi wakati wa masomo ya mtandaoni ili kuhakikisha usalama wa wafanyakazi, wazazi na wanafunzi wote. Wanafunzi wote wanatarajiwa kutumia masomo ya mtandaoni kwa njia yenye heshima, ya kisheria, na kujali hisia za wengine.

## Matumizi Yanayofaa ya Teknolojia

Kuna tovuti kadhaa ambazo zina nyenzo za kuchukiza, haramu, zisizofuata maadili na zisizofaa ambazo hazipaswi kutazamwa na wanafunzi. Wilaya ya Shule ya Lansing itafanya kila jaribio linalowezekana kuzuia tovuti hizi hata hivyo; inatarajiwa kwamba wanafunzi watatafiti kwenye wavuti wakitumia tovuti ambazo zinatumika kwa maudhui ya kozi hiyo. Tutafanya kazi kwa kushirikiana na wazazi kwa mwaka mzima, na tutakuwa na uwasilishaji maalum kuhusu Usalama wa Mtandaoni unaotolewa na ruzuku yetu ya STAR kwa wafanyakazi na wazazi wote kwa kuwa inahusiana na usalama kwenye intaneti.

## Matarajio na Adabu za Wanafunzi

### Matarajio ya Kila Siku ya Wanafunzi katika Masomo ya Mtandaoni

- Wanafunzi wanapaswa kuangalia kazi kwenye madarasa yao ya mtandaoni kila siku.
- Wasiliana kuhusu maswala ya muunganisho, ufikiaji wa mtandaoni, au maunzi mara moja kwa walimu wao.
- Kamilisha kazi/miradi yote kwa wakati.
- Hudhuria mikutano jinsi ilivyopangwa, na ushiriki kikamilifu katika vikao vya darasa.
- Fuata miongozo sawa ya kitabia kulingana na kijitabu cha wanafunzi wakati wa masomo ya mtandaoni (yaani hakuna lugha ya matusi, vitisho/, dhuluma, kufuata, n.k.).
- Wasiliana na mwalimu wako kupitia HMH (K-8), Michigan Virtual (9-12), au barua pepe ikiwa unapata matatizo ya kukamilisha kazi.
- Wanafunzi wote watatarajiwa kutoa kazi ambayo inategemea sifa zao na kutaja vyanzo ipasavyo inapohitajika. Wanafunzi ambao wananakili kazi za wengine wakijua au kuruhusu wengine kutumia kazi zao watakabiliwa na michakato ya kinidhamu kulingana na kanuni za maadili mema ya mwanafunzi.
- Wanafunzi na wazazi wanahimizwa kumjulisha mwalimu/msimamizi wa mtoto wao iwapo masuala yoyote ya usalama yatatokea wakati wa masomo.
- Wanafunzi wanawajibika kuhakikisha kuwa hakuna majina ya watumiaji au manenosiri yanayoshirikiwa na wengine wakati wa masomo ya mtandaoni.

### Adili ya Wanafunzi Wakati wa Masomo ya Mtandaoni

- Jiunge na vikao kwa wakati na ubaki katika hali ya kimya hadi maagizo yapokewe kutoka kwa mwalimu.
- Kipengele cha mazungumzo ni cha umma, na kila mtu anaweza kuona unachoandika!
- Kurekodi skrini na kupakia kwenye mitandao ya kijamii imepigwa marufuku kabisa.
- Jiepushe na mazungumzo ya kibinafsi.

- Wanafunzi wanapaswa kujaribu kuingia mtandaoni kwa kila mkutano wa darasa katika mazingira tulivu, yasiyokuwa na usumbufu ambayo yana mandharinyuma ambayo hawajali wengine wakiona.
- Lazima wanafunzi wavae mavazi yanayofaa kulingana na kanuni za shule za maadili mema wakati wa masomo ya mtandaoni.
- Wanafunzi wanapaswa kujaribu kuwezesha video ili mwalimu aweze kukuona pamoja na wanafunzi wenzako.
- Hakikisha kuwa unatoka kwenye vikao vya video.
- Wanafunzi hawapaswi kujiunga na vikao vya video ambavyo hawajaalikwa.
- Jiepushe na utumiaji wa vifaa vya kucheza, michezo ya video, na simu za rununu wakati wa masomo ya mtandaoni.

## Hatua ya Kinidhamu

### Hatua ya Kinidhamu kwa Tabia Isiyokubalika Wakati wa Masomo ya Mtandaoni

- Usumbufu katika kikao cha mtandaoni unaweza kusababisha mwanafunzi kuondolewa kutoka kwa sehemu au kikao chote.
- Wanafunzi ambao wameondolewa kwenye vikao vya wakati halisi kwa sababu ya tabia ya usumbufu hawawezi kupata sifa yoyote kwa shughuli hiyo, kazi ya darasa, tathmini, au ushiriki uliofanyika wakati hakuwepo.
- Usumbufu unaorudiwa utaripotiwa kwa msimamizi na inaweza kusababisha kuondoshwa kutoka kwa vikao vya wakati halisi.

### Tabia ambazo Zinaweza Kusababisha Hatua ya Kinidhamu

- Kurudia kuweka sauti mara kwa mara baada ya mwalimu kukunyamazisha.
- Kushiriki katika maonevu ya mtandaoni na unyanyasaji.
- Kukataa kufuata sheria za darasa ya mtandaoni zilizowekwa na mwalimu.
- Kuvaa vibaya darasani (nguo za kuonyesha uchu, ujumbe usiofaa kwenye mavazi).
- Kuendeleza ajenda ya kisiasa ya chama fulani isipokuwa iwapo inalingana na mtaala.
- Kudanganya au ulaghai.

## Majukumu ya Wazazi/Walezi

Kama mzazi/mlezi wa mwanafunzi wa mtandaoni, ni muhimu utambue jukumu muhimu unaloshiriki katika mafanikio ya jukwaa la masomo ya mtandaoni. Tunatambua kuwa kunaweza kuwa na vizuizi kadhaa na vipaumbele vingine kwa wanafunzi kuhusu kufanya kazi mtandaoni na hamasisho na msaada wako utakuwa muhimu kwa kuwafanya wanafunzi wawe na motisha wakati wa uzoefu wa mtandaoni. Walimu na wafanyakazi wa usimamizi watadumisha mawasiliano ya mara kwa mara na wazazi na walezi kuhusu utendaji wa wanafunzi sawa na masomo ya ana kwa ana. Tafadhali endelea kusaidia Lansing School District kwa kumruhusu mwanafunzi ahudhurie kila siku masomo ya mtandaoni.